

ALIYE MKUU KULIKO SULEMANI YUPO HAPA

 Asanteni, sana. Habari za jioni, marafiki. Nina furaha kuwa hapa usiku wa leo, nikifurahia tu kupeana mkono kidogo na ushirika na rafiki yangu wa kale, Ndugu G. H. Brown. Sijamwona kwa miaka. Yeye ni mmoja wa we—wenzangu wa mwanzoni, wa Arkansas, tulipokuwa kwenye Mtaa wa Victor wa 505 kule.

² Ninakumbuka, Ndugu Brown, usiku ambao yule mama katika orofa ya chini, kwa mgongo wake, akitambaa kwa mgongo wake, akiwa na ninii yake. . . Amepoteza akili yake, naye alikuwa katika hali mbaya sana. Baadaye, nilimkuta huko karibu na Jonesboro mahali fulani, akiwa na akili timamu, pamoja na mume wake, akiwa tu mzima alivyoweza kuwa.

³ Ndugu fulani alikutana nami tu hapa, nikamsalimia tu kwa mkono. Alikuwa anazungumza kuhusu kuwa mahali fulani, mke wake alikuwa na tezi, ninaamini, kwenye koo lake. Aliponywa katika mkutano. Angali ameponywa.

⁴ Mungu ni wa ajabu, sivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Tunashukuru sana kwa hilo. Tunapaswa kuwa, ambavyo ndivyo tulivyo, watu wenye furaha kuliko wote duniani, watu wa Mungu, wachangamfu, katika njia kwamba hatuogopi mauti. Mnajua, Kristo alishinda kila kitu, hata mauti, hata hofu ya mauti. Naam. “Ee kifo, u wapi mwiba wako? Kaburi, wapi ushindi wako? Lakini shukrani kwa Mungu Yule ambaye hutupatia ushindi kupitia Bwana wetu Yesu Kristo.” Jinsi tunavyompenda kwa sababu ya hilo!

⁵ Maskini dada huyu kutoka Florida, ninaamini, alisema, au mahali fulani hapa, aliyeimba ule wimbo: *Kushuka Kutoka Utukufuni Mwake*. Huo ndio wimbo ninaoupenda sana, ulioandikwa na rafiki yetu, Ndugu Booth-Clibborn. Nafikiri unaeleza kabisa Ungu Wake mkuu leo hii, katika siku ambapo watu wanajaribu kumfanya Yeye nabii tu au—au kiongozi fulani. Na mimi ninafikiri hiyo inaonyesha kile Yeye alichu, na mimi kwa kweli ninaupenda wimbo huo.

⁶ Sasa, mnajua, na kwa hiyo sehemu mbaya kuhusu mambo haya, mikutano hii si mirefu vya kutosha. Tunapata tu kukutana mmoja na mwenzake, na kusema “jambo,” na halafu inatubidi kuondoka tena. Lakini kwa kweli nimetazamia kuja huku chini.

⁷ Nitawaambia jambo fulani dogo. Sikusema hilo kama dokezo hivi majuzi usiku, kuhusu mimi kuwa na ile ndoo ya sukari ya rojorojo ya mtama ambayo yule dubu mdogo

aliingia ndani yake. Lakini mtu fulani usiku wa leo alinilipa, walinitumia gudulia la sukari rojorojo ya mtama. Asanteni, na nitahakikisha kwamba huyo dubu haipati hiyo. Nitamfanya mke wangu aniokee sinia nzima ya biskuti, na nitaziingilia moja kwa moja. Naam, bwana, kwa kweli ninapenda mtama.

⁸ Billy, mwanangu, ndio kwanza aniambie, kasema, “Baba, walikusanya sadaka ya upendo kwa ajili yako.”

⁹ Nilimwambia huyu mhubiri kwamba sikutaka hiyo. Unaona, sikuja kwa ajili ya hiyo, enyi watu. Nilikuja kuwasaidia, kujaribu kuwasaidia. Lakini hakuna njia kwangu kurudisha hiyo. Na ikiwa mtu yeyote anajua yeyote hapa ambaye yuko vibaya sana, mtu fulani, mwanamke mjane au kitu fulani, wanayo hiyo. Kwa hiyo asanteni sana. Unajua, Biblia ilisema, “Kadri mliyomfanyia aliye mdogo kuliko wote,” huyo ni mimi, “wa hawa wadogo, mmenifanyia Mimi.” Na mimi ninaomba kwamba Mungu atawabariki kwa ajili ya hilo, na kwamba Yeye—Yeye atawabariki. Nitawaambia, kama hakuna mtu aliye katika hali mbaya, anayeichukua, nitaiweka katika kazi ya umishenari kwa ajili ya huduma za nchi za kigeni. Ninaenda huko, mwenyewe, kwa hiyo ninajua inatumika vizuri.

¹⁰ Na kwa hiyo basi nijaribu kuleta Ujumbe huu wa ajabu wa—wa neema ya Mungu ambao umeletwa kwetu katika siku hizi za mwisho, Ujumbe, vizuri zaidi ni juavyo kuuleta Huo, na ni Ujumbe ule ule niliohubiri miaka mingi iliyopita. Sijauacha hata inchi moja, kwa sababu huwezi. Kama ningeuondokea, ingenibidi kutoka nje ya Biblia. Unaona? Kwa hiyo ni kutoka kwenye Biblia. Na mimi ninaamini kwamba, “Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa katikati yetu.” Na Waebrania 13:8 inasema, “Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.” Ninaamini hilo.

¹¹ Sasa, nilikuwa ninawazungumzia leo, wakati wa adhuhuri, juu ya Ujumbe wa Injili. Nilifurahi kumwona Ndugu Tracy Boutliere hapa, na yule ndugu hapa. Na, mimi, na wewe unajua jinsi ninavyojisikia kusimama hapa juu? Mimi—mimi kwa namna fulani ninajibana nisihubiri usiku wa leo, juu ya msingi wa hawa wahudumu wazuri wote kuwa hapa. Kwa hiyo ninaenda tu kuzungumza kidogo kuhusu Bwana Yesu, juu ya ufunuo Wake, mkubwa wa Yeye leo hii, na kuhusu nguvu Zake kuwaponya wagonjwa.

¹² Ndipo mwanangu akaja, muda mfupi uliopita, na akagawa kadi za maombi, na sisi tunataka kuomba wagonjwa usiku wa leo. Nanyi mnao wanaume hapa wanaoweza kuhubiri Injili; wamehubiri, juma hili lote. Na mimi nipo hapa kujaribu kufanya sehemu yangu, kuonyesha shukrani zangu kwa uaminifu wenu kwa Yesu Kristo, kwa kuwaomba wagonjwa.

¹³ Na sasa kabla hatujafungua Kitabu, hebu tuzungumze na Mwandishi wa Kitabu.

¹⁴ Wakati fulani uliopita, kulikuwa na mtu aliyeniambia. Nilikuwa nikizungumza kuhusu somo fulani katika Biblia, na lilikuwa ni somo lenye kilindi sana ambalo lina ubishi mwingi sana kuhusu, na juu ya Logos, na kadhalika. Ndipo yeye—yeye akaniangalia. Na mimi nilikuwa pamoja na Ndugu Jack Moore, na tulikuwa tunateremka chini Ziwa Cross, huko Shreveport, Louisiana. Basi mtu huyu alinitazama, ndipo akasema, “Wewe hujui tu Biblia yako.”

¹⁵ Nikasema, “Bali ninamjua Mwandishi vizuri sana. Na nina hakika, kama nikimpenda Yeye na kumjua Yeye vizuri sana, Yeye atalifunua Neno Lake kwangu.”

¹⁶ Kwa hiyo hebu tuzungumze na Mwandishi sasa, tunapoinamisha vichwa vyetu. Sasa huku tukinyamaza. Pia, kumbukeni, ndani ya mioyo yetu sasa, hivi kuna haja usiku wa leo miongoni mwetu, ambayo ungetaka Mungu aikumbuke, kwamba unaombea kitu hiki fulani, labda mpendwa fulani kumjia Kristo, usiku wa leo, labda mtu fulani apate kuponywa, ama haja nyingine? Ishikilie niani mwako, na uinue mikono yako kwa Mungu, useme, “Bwana, ikumbuke haja yangu.” Ni wote, kila mahali. Jinsi huu ulivyo ulimwengu mhitaji!

¹⁷ Bwana Yesu, tunakuja tukikukaribia Wewe katika lile Jina linalojitosheleza kwa yote, tukijua hili, kwamba tumeahidiwa kwamba maombi yetu yatasikiwa. Kasema, “Kile mwombacho katika Jina Langu, mtapewa.” Na sisi tunaleta haja hizi zote, usiku wa leo, juu mbele za Enzi nyeupe ya lulu ambapo Dhabihu iliyolowa Damu imewekwa, Yeye azisameheaye dhambi zetu zote, na huponya magonjwa yetu yote. Na sisi tuna shukrani sana Kwako, usiku wa leo, kwa ajili ya majaliwa haya makubwa tuliyo nayo, na pamoja na Neno la Mungu, ambalo haliwezi kushindwa. Japo Mbingu na nchi zinapita, Neno haliwezi kushindwa. Na Neno ni Mungu. Na Yeye ameahidi kwamba Yeye atasikia na atajibu maombi yetu. Sasa tuna hakika kwamba tunapata kile tunachoomba. Na mkono wangu umeinuliwa, pia, Bwana. Jibu, usiku wa leo, haja zetu.

¹⁸ Tunataka kukushukuru Wewe kwa ajili ya kile ambacho Wewe umekuwa kwetu, katika mkutano huu, kote kupitia maisha. Na pia tunakushukuru Wewe kwa ajili ya kile Wewe ulicho kwetu sisi, kuwa katika siku za usoni. Na katika majira ya kufa kwetu, kama Wewe utakawia, tunajua Wewe utakuwa ndiye me—merikebu ya kale ya Sayuni, Wewe utakuwa ndiye Mabawa yanayong’aa, Wewe utakuwa ndiye Nyota ya Asubuhi inayoangaza bonde la kivuli cha mauti, Wewe utakuwa ndiye Yule ambaye atatubeba kuvuka mto, kuingia katika ile Nchi mashuhuri ya ahadi. Tumeridhishwa na hayo, Bwana.

¹⁹ Usiku wa leo, wakiketi miongoni mwetu ni wanaume, wenye mvi na walioinama kwa sababu ya umri, na miaka mingi iliyopita nilipokuwa mvulana mwenye dhambi, walikuwa wakisimama kwenye pembe za barabara wakipiga vita vizuri vya imani, kwa ajili ya Ujumbe huu hasa tunaajaribu kupigania usiku wa leo. Baba Mungu, tuna shukrani wanaume hawa wangali wanaishi, kama shuhuda za imani hii kuu iliyokabidhiwa watakatifu mara moja. Tujalie daima kupigania hiyo na kuwa waaminifu kwa mahali petu pa wajibu, hata Yesu atakapokuja.

²⁰ Sasa tunakuomba Wewe uyabariki Maneno ambayo tunasoma, na kile tunachosema usiku wa leo. Jalia Hilo lianguke kwenye udongo wenye rutuba ambao utazalisha utumishi, kwamba hakutakuwa na mwenye dhambi mmoja katika jengo hili, ambaye atatoka hapa, ambaye hataokolewa. Jalia kila mtu mgonjwa aponywe. Naomba kusiwe na mtu mmoja mnyonge miongoni mwetu mwishoni mwa ibada. Ninajua huo ni mlima mkubwa unaosimama mbele zetu. Bali Wewe ulisema katika Injili Yako, kulingana na Marko Mtakatifu 11:22, “Ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka,’ na usione shaka moyoni mwako, bali uamini kwamba kile ulichosema kitatimia, utapata kile ulichosema.” Sasa tunaamini hilo.

²¹ Ulisema, “Wakati unaposimama kuomba, amini, samehe.” Na sisi tunaomba kwamba Wewe utatusamehe makosa yetu, kama ambavyo tumewasamehe wale waliotukosea sisi, hata kusiwe na chochote cha kuzuia maombi yetu yasijibiwe.

²² Pia, Bwana, naomba, ikitokea kwamba kamwe hatutakutana hivi tena katika mkutano mwingine, labda mwaka mmoja kuanzia sasa ama wakati wowote utakapokuwa, tunajua kunakuja mkutano mmoja mkubwa sisi sote tunaenda kuwepo, na hiyo ni Karamu ya Arusi. Ee Mungu, jalia kusiwe na mmoja wetu atakayekosekana kwenye wakati huo. Hadi wakati huo, tudumishe wenye afya na furaha, kukutumikia Wewe. Katika Jina la Yesu Kristo tunaomba hayo. Amina.

²³ Sasa, kuombea wagonjwa, si—sitoki kuingia kwenye kuhubiri. Kama nilivyosema, ni—ni upako tofauti; Roho yule yule, mkondo tofauti tu unaosafiria.

²⁴ Na sasa ninataka kusoma kifungu kinachojulikana cha Maandiko, na Maandiko machache hapa ningependa kurejea, kabla tu hatujaitisha mstari wa maombi. Pia ninajua kuna joto, na sitaki kuwaweka kwa muda mrefu.

²⁵ Na mimi ninajua kufungwa kwa mkutano, juma kubwa, na jinsi mlivyojaa kwa kiwango hasa sasa, na mnaenda nyumbani kuwa na wakati mzuri. Hutaki kuenda nyumbani ili tu kuwa na wakati mzuri kufurahia baraka za Mungu, bali kuenda nyumbani kuchukua kile ambacho umejifunza na kukipitisha kwa mtu mwingine. Na hebu watoto wa

mkutano huu, waliozaliwa tena, katika mkutano huu, mwaka ujao walete vilembwekeza pamoja nao; kumaanisha kwamba wewe umemshawishi mtu mwingine, nao wakamshawishi mtu mwingine, nao wakamshawishi mtu mwingine kuja kwa Bwana.

²⁶ Sasa hebu tufungue usiku wa leo katika Marko Mtakatifu, mlango wa 12. Na ninataka kuanza kusoma kuanzia kifungu cha 38 cha Mtakatifu...cha Marko Mtakatifu 12, nikisoma kuteremka pamoja na kifungu cha 42, vyote pamoja. Na, kwa kawaida, kama ilivyo desturi mara nyingi, tunasimama tunaposoma Neno la Mungu, lakini kwa kuwa mmesongamana sana usiku wa leo, tutaacha hiyo, na kuketi tu kwa uchaji na kusikiliza Neno. Ikiwa una Biblia, nifuate ninaposoma.

Hapo baadhi ya waandishi na Mafarisayo wakamjibu, wakasema, Mwalimu, twataka kuona ishara kwako.

Akajibu, akawaambia, Kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta ishara; wala hakitapewa...ishara, ila ishara ya nabii Yona.

Kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi; ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi.

Watu wa Ninawi watasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, nao watawahukumu kuwa wamekosa; kwa sababu wao walitubu kwa mahubiri ya Yona; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona.

Malkia wa kusini atasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, naye atawahukumu kuwa wamekosa; kwa sababu yeye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani, na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.

²⁷ Huenda nikatumia hili kwa ajili ya fungu: *Aliye Mkuu Kuliko Sulemani Yupu Hapa*. Kama tukisoma sehemu za nyuma za Maandiko, yanayotangulia haya, tunapata kwamba kwa namna fulani inafungamana na kile tulichokuwa tukisema jana jioni.

²⁸ Wakati Kristo alipokuja duniani, Yeye aliwajia Walio Wake, na Walio Wake hawakumpokea. Na hao Wayahudi walifunzwa na Maandiko, kuhusu aina ya tabia ambayo huyo Masihi angekuwa. Na Masihi alikuwa awe nabii, kulingana na sheria zao. Musa alisema, “Bwana Mungu wako atamwinua Nabii, kama mimi, na Kwake watu watashikilia; na kama hawatamsikia Yeye, watakatiliwa mbali kutoka kwa watu.”

²⁹ Unaona, Maandiko kamwe hayaachi wakati wowote bila ya utambulisho dhahiri, kusudi tuweze kujua ni wakati gani tunaishi.

³⁰ Hata katika Mathayo Mtakatifu 24, Yesu akizungumza kuhusu wakati wa mwisho, Yeye alisema, “Sasa jifunzeni methali kutoka kwa mtini.”

³¹ Tena Yeye akasema kile kitakachokuwa ishara ya yale maswali matatu. “Ni wakati gani ambapo hakutakuwa na jiwe litakalosalia juu ya jingine, la jengo? Ni nini ishara ya Kuja Kwako, na mwisho wa ulimwengu?” Na Yeye alijibu maswali yote matatu. Mara nyingi, watu huyaweka yote matatu kama swali moja, bali wao walimwuliza Yeye maswali matatu. Aliyajibu maswali hayo matatu. Lakini Yeye alitoa, hapo, ishara, kwa sababu, Wayahudi wanatafuta ishara. Na ni kwa nini wanatafuta ishara? Ni kwa sababu waliagizwa kufanya hivyo. Myahudi daima aliamini mambo ya kimbinguni.

³² Hata chini ya torati, kwamba alipokuwapo mwotaji, au nabii, ambaye alitoa ujumbe ambao kidogo haukueleweka, ama hawakuwa na hakika nao sana, walikuwa na njia ya kuchunguza kama ujumbe huo ulikuwa sahihi au la. Walimchukua huyu mwotaji, ama nabii, wakampeleka chini kwenye hekalu ambapo U—Urimu Thumimu, ilikuwa ni deraya ya kifua iliyoning’inia, ama iliyokuwa kifufu mwa Haruni, ambayo iliwakilisha makabila yote ya Israeli. Ndipo nabii huyu akatabiri, au mwo—mwotaji akasimulia ndoto yake.

³³ Na haijalishi jinsi ilivyoonekana halisi, kama ndoto hiyo au unabii haukuakisi nuru ya kimbinguni, namna fulani ya mkusanyiko kama upinde wa mvua katika hiyo, ambayo iliitwa Urimu Thumimu, ujumbe huo ulikataliwa. Wa asili lazima ajibu kwa wa kimbinguni, na wa kimbinguni lazima ajibu kwa wa asili. Hivyo basi, katika Agano la Kale, Urimu Thumimu ilikuwa ndiyo kipimo, kama maneno yalikuwa kweli au sivyo. Hiyo ilikuwa ni chini ya ukasisi wa Lawi.

³⁴ Lakini Mungu kamwe hakutuacha bila Urimu Thumimu, kwa sababu Neno Lake usiku wa leo ndilo Urimu Thumimu. Haijalishi jinsi ujumbe unavyosikika wa kupendeza, ama jinsi ndoto inavyosikika kuwa nzuri, hata hivyo, isipotoa nuru kwenye Urimu Thumimu, Neno la Mungu, kwa ushauri wangu, achana nayo, kwa sababu Mungu hashuhudii. Kwa sababu, Kitabu hiki ndicho ufunuo mkamilifu wa Yesu Kristo.

³⁵ Sasa, Yesu alikuwa amekuja na alikuwa amefanya hasa vile Maandiko yalivyosema Yeye angefanya.

³⁶ Na wakati mtume Petro, kama tulivyozungumza jana jioni, akiagizwa na baba yake, na walimu, kwamba kutakuwa na kuinuka kwa Masihi, na kwamba Masihi huyu atakuwa ni Nabii. Sasa kwa miaka mia nne, kuanzia Malaki, hawakuwa wamekuwa na manabii. Na hapa alikuwepo Mtu ambaye wakati Yeye alipotembea huko, hajavalia tofauti hata, si kama kasisi fulani mashuhuri au padri, bali mtu wa kawaida tu. Na yeye asingemjua Masihi huyu kwa jinsi Yeye alivyovalia, bali

wangemjua Yeye kwa U—Uzima uliokuwa ndani Yake. Basi wakati Yesu alipomtazama na kusema, “Jina lako ni Simoni nawe ni mwana wa Yona,” ndipo huyo mtume alikuwa tayari kujisalimisha, kwa sababu alijua kwamba Yesu hakumjua. Sio tu kwamba Yeye alimjua, lakini Yeye alimjua baba yake pia, kwa hiyo alijua hiyo ilikuwa ni ishara ya Masihi.

³⁷ Tulimfuata pia Filipo, kumpata Nathanaeli. Akamleta huku, ambaye alikuwa ni m—mtu mwaminifu, aliyefunzwa sana katika Maandiko. Tunakuta kwamba labda Filipo alimweleza, njiani wakienda, yale yaliyokuwa yametokea. Lakini wakati alipomfikia Huyo, Yeye alimwita, kasema, “Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake.”

Akasema, “Ulinijua lini Wewe, Rabi?”

³⁸ Kasema, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nalikuona.”

Ndipo yeye akasema, “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu, Mfalme wa Israeli.”

³⁹ Ndipo basi kwa taifa la Wasamaria, huko maskini mwanamke huyu katika Sikari. Jinsi ambavyo yeye katika hali yake kama mwanamke mwenye sifa mbaya; lakini wakati Nuru hiyo ya Injili ilipotanda kupitia njia yake, na Yeye akamwambia kuhusu dhambi yake na kile alichokuwa amefanya, mwanamke alisema, “Bwana, Wewe ni, lazima ni nabii. Na sisi tumefunzwa, na tunajua kwamba ajapo Masihi, Yeye atatuambia mambo.” Hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi.

⁴⁰ Ndipo tukajifunza kwamba Yeye hakuifanya ishara hiyo mbele za Mataifa, bali alitabiri kwamba itafanywa hapa katika siku za mwisho, na Roho Mtakatifu. Basi, kumkufuru Huyo, haingesameheka.

⁴¹ Kama Yeye alivyosema ingekuwa kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, tulipoona kwamba wakilisho la Mungu ndani ya mtu, mwanadamu, aliyekula nyama ya ng’ombe, au ndama, hasa, na kunywa maziwa kutoka kwa ng’ombe, na kula mkate, naye alimwita Huyo, “Elohimu,” Mungu mkuu, Muumba.

⁴² Mungu alifanyika mwili katika mwili wa Yesu Kristo.

⁴³ Basi leo hii Yeye yuko ndani ya kanisa Lake, katika umbo la Roho Mtakatifu, angali Mungu. Na yule mtu katika mwili, aliyewakilishwa kwenye wakati wa mwisho kabla ulimwengu wa Mataifa kutekelezwa kwa moto, kwamba Mungu atakuwa katika mwili wa kibinadamu, akifanya jambo lile lile, kujithibitisha Mwenyewe kwa Mataifa. Na sisi tulimwona Yeye akija miongoni mwetu, jana usiku, na kufanya jambo hilo.

⁴⁴ Kwa hiyo sasa Yesu alikuwa akiwakemea watu hawa, usiku wa leo, kwa sababu ya kutokuamini kwao, kwa sababu walipaswa kuwa wamefundishwa Kimaandiko. Lakini desturi za siku hiyo zilikuwa zimewavuta watu kutoka kwa

Biblia, Maandiko. Yesu alisema, “Nyinyi kwa mapokeo yenu mmezitangua Amri za Mungu.”

⁴⁵ Na ninashangaa usiku wa leo, kama Yeye angesimama juu ya udongo huu wa Marekani, kama Yeye asingesema jambo lile lile kwa wengi usiku wa leo. Kwa mapokeo ya wanadamu, mmezichukua Amri za Mungu na mmezitangua, kwa kuhubiri kwamba, “siku tu za miujiza zimepita,” na kadhalika, kama wafanyavyo. “Wakiwa na mfano wa utauwa,” ambao nabii alisema ingekuwa katika siku za mwisho, “bali wakikana Nguvu zake.”

⁴⁶ Tunaona, katika hili, kwamba Yeye alikuwa anawakemea, kwa sababu iliwabidi kuangalia ishara na kuamini ishara. Nuhu aliwapa ishara. Mungu daima katika kila wakati alishughulika na mwanadamu kupitia ishara, kwa sababu Yeye ni wa kimbinguni. Na mahali alipo Mungu wa mbinguni, hapana budi kuwepo na mambo ya kimbinguni yakiendelea.

⁴⁷ Ndipo tunaona, katika siku za Nuhu, wale walioamini ujumbe wake na kuingia ndani, waliokolewa, na wale waliokataa ujumbe wake waliangamia. Aliwapa ishara ya kujenga safina.

⁴⁸ Katika siku za Musa, kunena kwa Mungu kupitia midomo ya mwanadamu kungeweza kuwaita nzi, viroboto, vyura, kufunga mbingu, kuleta giza, kupitia nabii ambaye alithibitishwa vilivyo. Wale walioamini na kutoka Misri, kuvuka mstari wa utengano wa Bahari ya Shamu, waliokolewa. Wale waliokuwa upande ule mwingine, waliangamia.

⁴⁹ Na Yesu alikuwa akiwaambia. Walimwita Yeye, “Beelzebuli,” wakidai kwamba Yeye alikuwa akisoma nia za watu. Au wengine leo hii, wangesema, “Ni kuwasiliana kimawazo.” Lakini mtu yeyote mwenye akili ambaye anajua chembe yoyote ya kuwasiliana kimawazo, anajua kwamba mambo ambayo tunayaona hayawezi kuwa kuwasiliana kimawazo.

⁵⁰ Hivi majuzi, huko Tucson, kulikuwa na maskini ndugu Mbaptisti, na yeye alitoka nje, nikimleta maskini Rebekah wangu nyumbani kutoka shuleni, nikibeba vitabu vyake. Na yeye akaenda kwenye mkutano. Anamwita baba yake, mmishenari huko chini Meksiko, mtu mwema, mfanyakazi mwenza wa Billy Graham; ndipo akasema, “Baba, harakisha nyumbani, tumeona nguvu za Bwana Yesu zikidhihirishwa.”

⁵¹ Akasema, “Mwanangu, una shida gani?” Akampigia simu kwa masafa marefu. Na yeye akaeleza kilichotukia. Akasema, “Hayo yanaweza kuonekana katika mkutano wowote duni.”

⁵² Na kijana huyo akaketi hapo kidogo. Akasema, “Baba, ninakupenda. Umekuwa baba yangu, na umejaribu kunilea vizuri. Lakini sijui kama tungeweza kubonyeza swichi turudi nyuma kwenye wakati ambapo Yesu wa Nazareti alifanya jambo

lilo hilo kwenye kingo za Galilaya, kama ungekuwa tayari kuita huo mkutano duni?” Mtu huyo aliondoka mahali pake pa kazi, na akaja na akashawishika.

⁵³ Unaona, Yesu alikuwa anajaribu kuwaambia, “Ikiwa sizifanyi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Ni nani kati yenu awezaye kunihukumu Mimi kwamba nina dhambi, ambayo ni kutokuamini? Ikiwa sijatimiza maneno yote yaliyoandikwa kunihusu Mimi, basi unaweza kuninyoshea kidole; bali nimefanya yale hasa Maandiko yaliyosema ningefanya.”

⁵⁴ Loo, kama kanisa lingeweza tu kuchukua msimamo huo, usiku wa leo, kama mwakilishi wa Yesu Kristo, na kusema, “Tumepungukiwa wapi? Mungu, ninataka kuishi kuona siku ambapo kanisa la Yesu Kristo linaweza kuwa moja katika kusudi na moyo na mwili, likisimama katika nguvu kamili zilizotiwa upako wa Roho Mtakatifu, kutenda na kufanya kama Yesu Kristo alivyofanya, wakiwa na Mungu ndani yao, pia.”

⁵⁵ Sasa Yeye alianza kurudi nyuma na kuwakemea. Walijua kwamba Mungu, katika vizazi vyote, hutuma karama. Na wakati Mungu anapotuma karama duniani, na inakataliwa, taifa hilo au kizazi hicho huingia hukumuni. Na ikiwa Mungu anatuma karama na inapokelewa, kizazi hicho kinabarikiwa.

⁵⁶ Nilikuwa nikiwaza usiku wa leo, nilipokuwa ninakuja huku, nikiwaza juu ya hili, kwamba, “Ingekuwaje kama Marekani yote, usiku wa leo, ingeamini karama ya Mungu ambayo tumepokea?”

⁵⁷ Yesu hapa anarejea kwenye wakati wa—wa Yona, au Yona kwa kweli ni kile alichu. Na watu wengi humlaumu Yona, na wanasema kwamba Yona alikuwa... Unasema, “Alikuwa ni Yona. Yeye alifanya *hili, lile,*” kwa sababu Yona, tunafikiri, alitoka nje ya mapenzi ya Bwana.

⁵⁸ Lakini hebu nijaribu kutetea hilo kuwa la haki, usiku wa leo. Biblia ilisema, “Hatua za mwenye haki huongozwa na Bwana.” Wakati mwingine, Yeye hutufanya kutenda mambo kinyume sana na tunavyofikiria; lakini sisi daima, ikiwa tunafuata uongozi wa Roho, daima tuko katika mapenzi Yake. Mungu hufanya kile Yeye anachotaka kufanya. Alimwinua Farao kwa kusudi lile lile; na kuita, kasema Yeye alimpenda Yakobo na alimchukia Esau, kabla hawajazaliwa. Sasa kusudi la Mungu halina budi kutimia. Je! mfinyanzi... ama udongo unaweza ukamwambia mfinyanzi, kama tunavyopata katika Warumi 8 na 9.

⁵⁹ Angalia, tunapata hapa kwamba Yona aliamriwa na Mungu kuenda huko chini Ninawi, kuhubiri, na kusema kwamba katika siku arobaini mji huo utaangamia, kwa sababu Ninawi ulikuwa ni mji mkuu uliojaa dhambi, nchi ya ukafiri. Waliabudu sanamu. Walikuwa, kazi yao kubwa ilikuwa ni kuvua samaki, kwa sababu walikuwa kando ya ufuo wa bahari. Na mkazi wa—wao alikuwa... kazi zao, ilikuwa ni kuvua samaki. Basi Yona, badala

ya kuchukua merikebu. . . Na labda merikebu haikuwa inaenda kwenye wakati huo hasa. Bali alipanda merikebu inayoelekea Tarshishi. Na sisi tunaona na kufahamu shida ambayo Yona aliingia ndani yake, huko nje baharini. Ninaamini kwamba yote hayo yalipangwa na Mungu. Bahari ilichafuka, ndipo Yona akasema, “Nifungeni mikono yangu na mnitupe nje ya chombo.” Na Mungu alikuwa na samaki aliyeandaliwa, kama tunavyoita “nyangumi,” na kummeza nabii.

⁶⁰ Miaka michache iliyopita, nilikuwa huko Louisville, Kentucky, wao—wao walikuwa na nyangumi kwenye. . . mifupa ya mmoja, juu ya—juu ya behewa. Naye maskini huyu Riki amesimama hapo, akiwa na miwani yake juu ya pua yake, na alionekana kuwa na elimu nyingi kuliko aliyokuwa na akili kudhibiti, alikuwa anajaribu kueleza kuhusu huyu nyangumi. Akasema, “Unajua, hekaya ya kale ya Biblia, kwamba nyangumi alimmeza Yona.” Alisema, “Hiyo ni hekaya tu ya uongo.” Kasema, “Kwa sababu, unaona, ingekuwa vigumu kwako kurusha mpira kupitia koo lake, ni dogo sana, na asingeweza kummeza mtu.”

⁶¹ Hiyo ilikuwa imepita kipimo sana kwangu kuweza kustahimili. Ni—nikamwambia, nikasema, “Bwana, ni—ninataka kusahihisha hilo.”

Akasema, “Ni kitu gani hicho?”

⁶² Na mimi nikasema, “Unaona, huenda yeye. . . Nyangumi huyo huenda hakuweza kummeza, lakini Biblia ilisema, kwamba, ‘Mungu alimwandaa samaki.’ Alijengwa maalum. Mungu alimfanya mkubwa wa kutosha kummeza.” Unaona? Ni—nilijihisi tu ninge kuwa ni msaliti wa Biblia kama sikutoa ushuhuda wangu, kuonyesha sura, maana watu wamesimama hapo wakicheka. Nakwambia, lilikuwa ni jambo tofauti wakati hilo liliposemwa, unaona, halikuwa la kuchekesha sana, niliposema, “Huyajui Maandiko. Maandiko yalisema, ‘Mungu aliandaa samaki.’ Alimfanya huyu maalumu.”

⁶³ Kama vile maskini msichana fulani wakati mmoja, akitoka kanisani, alisema alikuwa na furaha. Maskini nywele zake zimechanwa kurudi nyuma, na yeye alikuwa na wakati mzuri, akiimba sifa za Mungu. Kafiri kwenye kona alisema, “Ni kitu gani kinachokufurahisha sana, msichana mdogo?”

Akasema, “Ndiyo kwanza niokolewe, ninaenda Mbinguni.”

⁶⁴ Akasema, “Ni nini hicho ulicho nacho kwenye kwapa lako, kitu hicho wanachokiita Biblia?”

Akasema, “Ndiyo, bwana, ni hiyo.”

Kasema, “Huamini hiyo?”

Kasema, “Kila Neno lake.”

⁶⁵ Kasema, “Vema, nadhani unaamini ile hadithi kuhusu nyangumi kummeza Yona?”

66 Akasema, “Naam, bwana, ninaamini hiyo. Kama Biblia ilisema kwamba Yona alimeza nyangumi, ningeamini hiyo.”

67 Na yeye akasema, “Sasa unaendaje kuthibitisha kwamba—kwamba nyangumi alimmeza Yona, kwa njia yoyote nyingine ila kwa imani?”

Akasema, “Nitakapofika Mbinguni, nitamwuliza Yona.”

Akasema, “Basi vipi ikiwa Yona hayuko huko?”

68 Kasema, “Basi itakubidi wewe kumwuliza.” Kwa hiyo ilienda tu kuonyesha kile kilichokuwa kinaenda kutendeka, alienda njia ile nyingine. Na hiyo karibu inaonyesha hiyo.

69 Lakini ninaamini kuwa nyangumi alimmeza Yona. Sasa, huku mikono imefungwa, ndani ya tumbo la nyangumi, huko nje juu ya bahari, yapata urefu wa mikono arobaini kuenda chini.

70 Sasa nyinyi wanawake mnajua, kwa maskini samaki wenu wenye rangi ya dhahabu. Samaki huzungukazunguka majini, ili kupata chakula chake. Na baada ya kupata chakula chake, hujaza tumbo lake dogo kabisa, anaenda chini ya shimo na kutuliza maskini pezi lake huko. Unaona, anapumzika. Mapezi yake humshikilia juu. Na sasa amestarehe kwa sababu amechoka kutokana na kuzungukazunguka.

71 Hebu tuwazie samaki huyu mkubwa alifanya jambo lilo hilo. Wakati alipommeza nabii, anaenda chini kabisa, uzito wake mkubwa wa tani nyingi, analala kule chini sasa, huku nabii akiwa ndani ya tumbo lake. Naye nabii alikuwa angali hai. Yeye alimmeza. Na Yona hapana shaka aligeuka, chini ndani ya tumbo la nyangumi. Na, unajua, kila mahali alipotazama, aliweza kuona tumbo la nyangumi.

72 Na mara kwa mara nimewazia kuhusu watu, kusema, “Niliombewa jana usiku, lakini mkono wangu hauna tofauti. Niliombewa, na sisikii vizuri hata kidogo.” Vema, unaangalia dalili, mradi tu unaangalia hizo. Kama mchungaji wako alikuombea, akakupaka mafuta, au mfumo wowote anaotumia wa Biblia ya Mungu, huna budi kuamini. Inakubidi kuamini hiyo.

73 Sasa sifikirii kwamba yeyote wetu hapa alikuwa na dalili nyingi kama Yona alizokuwa nazo, kwani, kila upande alioangalia, ilikuwa ni tumbo la nyangumi. Lakini unajua kile alichosema? Alisema, “Hizo ni ubatili na uongo.” Haendi kuamini hizo. Alisema, “Mara nyingine tena nitangaalia kwenye hekalu Lako takatifu.”

74 Sasa Yona alijua kwamba wakati Sulemani alipoweka wakfu hekalu, Mungu alithibitisha Uwepo Wake hekaluni, kwa kuingia kama Nguzo ya wingu, na kuingia ndani na kuenda huko nyuma ya Mahali Patakatifu, juu ya Kiti cha Rehema na juu ya sanduku, na kutulia. Na Sulemani akaomba, “Bwana, watu Wako wakiwa

katika matatizo, mahali popote, na watatazama mahali hapa patakatifu, na kuomba, basi Wewe uwasikie kutoka Mbinguni.”

⁷⁵ Sasa, kama Yona, chini ya hali hizo, angeweza kuwa na imani katika maombi ya mtu, mwanadamu, ambaye baadaye alirudi nyuma; na juu ya hekalu ambalo lilijengwa na mikono ya mwanadamu, ambalo Mungu alikuja ndani yake; na alikombolewa kutoka kwa hizo, dalili kama hizo; ni zaidi jinsi gani inavyotupasa sisi, usiku wa leo, chini ya hali yetu ndogo, moja kwa moja katikati ya Uwepo wa Mungu mkuu Mwenyewe, ambapo tunaona watu wakipona, wakiokoka, na kujazwa na Roho Mtakatifu! Usiangalie kuelekea hekalu la kawaida; bali angalia kuelekea hekalu lililoko Mbinguni, ambapo Kristo ameketi kwenye mkono wa kuume wa Ukuu, na nguvu, pamoja na Damu Yake Mwenyewe, kufanya uombezi juu ya maungamo yetu. Tunapaswa kuonea aibu udhaifu wetu. Sasa, mpaka utakapoweza kuwa na imani bora kuliko aliyokuwa nayo Yona, usimkosoe.

⁷⁶ Tazama, ndipo tunaona kwamba Mungu, chini ya maombi hayo na imani hiyo... Angeweza kuweka hema la oksijeni kule; sijui kile Yeye alichofanya. Lakini alikaa, kulingana na Neno la Kristo Mwenyewe, siku tatu mchana na usiku katika tumbo la huyo nyangumi. Halafu basi hebu tuliwazie, kuhusu, huenda ilikuwa yapata saa tano mchana, wavuvi wote walikuwa karibu tayari kuingia kwa ajili ya chakula chao cha adhuhuri, na walikuwa karibu wanachukua nyavu zao. Na hawa makafiri waliabudu wanyama, na mungu wa baharini alikuwa ni nyangumi. Na yapata tu katikati ya mchana, huyu hapa akaja mungu wa baharini akiingia, nyangumi, akautoa ulimi wake nje, ndipo nabii akatembea moja kwa moja akitoka katika kinywa chake. Si ajabu walitubu, hakika, kwa sababu mungu alitema nabii. Na yeye akapitia mitaani, akisema, “Katika siku arobaini mahali hapa pataangamizwa.” Unaona, Mungu anajua jinsi ya kufanya mambo.

⁷⁷ Sasa, walimwuliza Yesu ishara, na Yeye akawaambia kwamba, “Ki—kizazi kibaya na cha zinaa kinatafuta ishara.” Na, sasa, ninajua kuna tafsiri kwamba Yeye alimaanisha hao. Hiyo ni kweli. Lakini ninaenda tu kuliendeleza, likiwa na maana zaidi ya moja.

⁷⁸ Ni lini tulipowahi kuwa na kizazi kibaya na cha zinaa zaidi ya tulicho nacho sasa hivi? Kizazi kibaya na cha zinaa! Watakuambia, toka nje mtaani, waseme, “Je! wewe ni mponyaji wa Kiungu?”

“La. Kristo ndiye.”

⁷⁹ “Vema, kama wewe ni mponyaji, ama unaamini, unasema wewe ni mponyaji; ninamjua jamaa aliye hapa chini ni mgonjwa, njoo ukamponye. Ninajua unasema uliwafufua wafu; mtu

alikuwa na wewe ukamfufua? Tuna sehemu ya makaburi hapa iliyojaa hao hapa chini; tuthibitishie.”

⁸⁰ Kumbuka, huyo ni yule yule ibilisi wa kale ambaye alisema, “Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, amuru mawe haya yawe mkate.”

⁸¹ Ni yule yule ibilisi wa kale aliyeweka kitambaa juu ya macho ya Bwana wetu, katika ikulu asubuhi ile, akayafunika macho Yake, na wao wakachukua fimbo, wale askari walevi, wenye fujo, na kumpiga Yeye kichwani kwa hiyo, na halafu wakapitisha fimbo, mmoja kwa mwingine, na kusema, “Tunasikia kwamba Wewe unajua siri za moyo. Tunasikia kwamba Wewe ni nabii. Kama Wewe ni nabii, tabiri na utuambie ni nani aliyekupiga. Tutaamini basi.” Unaona, huyo ni yule yule ibilisi wa kale. Unaona? Mungu hamfanyii vitimbi mtu yeyote.

⁸² Ni yule yule ibilisi wa kale ambaye alisema, “Shuka kutoka msalabani. Hebu tukuone Wewe ukitenda mwujiza.” Ibilisi huyo anaishi leo.

⁸³ Naye Yesu alisema, kwamba, “Kizazi kibaya, kinyonge, cha zinaa kingetafuta ishara, nao wangeipata. Kwani kama Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi, siku tatu mchana na siku tatu usiku, ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa katika moyo wa nchi.” Basi ni ishara ya aina gani ambayo Yeye alikuwa akizungumzia? Ishara ya ufufuo. Na baada ya miaka elfu mbili ya kuhubiri Injili, miaka elfu mbili ya pingamizi, Biblia imepenya kupitia hizo zote. Na, usiku wa leo, Yesu Kristo yuko miongoni mwetu, katika nguvu za kufufuka Kwake, akifanya mambo yale yale ambayo Yeye alifanya wakati Yeye alipokuwa hapa duniani. Hiki ndicho kile kizazi kinyonge na cha zinaa.

⁸⁴ Yohana Mtakatifu 14:12, Yesu alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo yeye atazifanya pia.” Unaona? “Bado kitambo kidogo na ulimwengu, utaratibu wa kosmos, hautaniona Mimi tena, hata hivyo nyinyi mtaniona Mimi. Huyo ni asiyeamini, ulimwengu, utaratibu wa ulimwengu, utaratibu wa kanisa, hautaniona Mimi tena. Hata hivyo nyinyi mtaniona Mimi, mwaminio, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hadi mwisho wa ulimwengu.”

⁸⁵ Na kizazi hiki kibaya na cha zinaa tulicho nacho duniani, cha kudhihaki Neno la Mungu la asili, kudhihaki ka—kanisa, anapokea usiku wa leo ishara ya ufufuo. Kwa sababu, mambo ambayo Yesu Kristo anafanya leo hii, ndani ya kanisa, hakuna mtu ulimwenguni anayeweza kuyafanya nje ya Yesu Kristo. Na ni ishara kwamba Yeye yu hai usiku wa leo. Alifufuka kutoka kwa wafu, miaka elfu mbili iliyopita, na yu hai tu usiku wa leo kama Yeye alivyokuwa wakati Yeye alipotembea Galilaya. Amina. Ishara ya ufufuo!

⁸⁶ Ndipo tunaona, kuteremka chini, Yeye anarejea wakati wa Sulemani. Alisema, “Watu wa Ninawi walitubu kwa mahubiri

ya Yona, na hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona.” Alisema, “Tena kama katika siku za Sulemani, jinsi malkia wa Kusini alivyokuja kutoka pande za mwisho za dunia, kusikia hekima ya Sulemani, na aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa.”

⁸⁷ Unaona, wasingeweza kuelewa hilo. Walikuwa wenye uzito wa kuelewa. Isaya alisema, “Wana macho na hawawezi kuona, masikio na hawawezi kusikia.”

⁸⁸ Ninaenda kusema hili kwa upendo. Pentekoste, karibu inafikia njia iyo hiyo. Kitu ambacho Mungu aliahidi, kinapita moja kwa moja juu yetu, na tunakiacha tu kiende. Kilicho shida ya watu Wapentekoste, ni hiki, wameona mengi sana ya Mungu. . .

⁸⁹ Inanikumbusha methali ya kale, au hadithi niliyosoma wakati mmoja kuhusu mwandishi aliyekuwa ameandika kuhusu bahari, na alisema hakuwa amewahi kuiona. Kama tunavyosikia kwamba Stephen Foster, mwandishi anayependwa wa hadithi, aliandika kuhusu Mto “Swanee”, na kamwe hakuona Mto Suwannee. Naye mwandishi huyu alikuwa ameandika kuhusu bahari, na kamwe hakuwa ameiona bahari. Wakati mmoja alifunga safari kuenda baharini. Na njiani mwake alikutana na mzee baharia, baharia stadi, akipanda juu, akiwa na masharafa yenye mvi usoni mwake, na kiko chake cha gunzi la hindi kinywani mwake. Akasema, “Unaenda wapi, rafiki mwema?”

⁹⁰ Akasema, “Ninaenda baharini.” Akasema, “Mimi ni—mimi ni mshairi.” Akasema, “Ni—ninataka tu kuiona. Ninataka kuona mawimbi yake meupe wakati mawimbi ya baharini yanaporuka juu ya bluu. Ninataka kuona uakisi wa anga katika maji ya samawati, ninuse chumvi hewani. Ninataka kusikia shakwe wakilia na kupiga makelele, wanapoenda huku na huko kuvuka maji.”

⁹¹ Yule baharia hodari akatoa kiko chake cha gunzi la hindi kutoka kinywani mwake, akatema mate. Akasema, “Nilizaliwa ndani yake, miaka sitini iliyopita. Sioni chochote cha kupendeza sana kuihusu.” Kwa nini? Alikuwa ameona mengi sana kuihusu, ikawa ya kawaida kwake.

⁹² Na hiyo ndiyo shida na nyinyi Wapentekoste. Mnaona mengi sana ya sifa na baraka za Mungu, mpaka zinapita moja kwa moja kupitia kwenu. Lazima tuwe na kicho na mambo haya, na kuheshimu kila kitu ambacho Mungu anatupatia.

⁹³ Sasa, siku za Sulemani, kama mwanatheolojia yeyote, mtu wa Maandiko anajua kwamba huo ulikuwa ni wakati mzuri sana wa Waebrania. Hawakuwa na vita. Wao, ilikuwa karibu kama Utawala wa miaka elfu kwao. Siku kuu! Walijenga hekalu. Mataifa yote yaliwaogopa. Waliogopa kufanya chochote, kwa sababu wanajua kwamba watu walikuwa na moyo mmoja na nia moja. Mungu aliwapa kipawa, na walikiamini. Walikikubali, na kwa moyo mmoja na mapatano walifanya kazi nacho.

⁹⁴ Loo, kama sisi, watu wa Marekani wanaweza, usiku wa leo, wa Presbiteri wote, na Methodisti, na Baptisti, na Pentekoste, kurarua desturi yenu ambayo dhehebu lenu limejenga kuwazunguka, kutenganisha udugu, “inavyoonekana bila kuwa na imani.” Kama tungeweza kutoka kwenye hilo ganda la kale tulilo ndani yake, na tungeweza kuja pamoja na kukikubali kipawa cha Mungu, juu ya msingi kwamba Yeye alitupatia hicho, kingekuwa ngome bora ya kujihami na bomu kuliko zote nijuazo. Afadhali nisimame nyuma ya hiyo, ahadi za Mungu, kuliko ngome zote za kujihami na bomu ambazo wangeweza kujenga. Jinsi, ni taifa la namna gani, ni uamsho wa jinsi gani ungekuwepo, jinsi mataifa mengine yangeogopa kufanya chochote juu yake. Mungu ametupatia kipawa, lakini tunakidharau.

⁹⁵ Tunajaribu kukileta huku katika kundi dogo, na kusema, “Tunacho, na nyinyi hamna chochote kingine kuhusiana nacho, kwa sababu hamuoni kupitia miwani yangu.” Hatupaswi kufanya hivyo. Si sahihi. Mradi tu ibilisi anaweza kuwafanya mpigane nyinyi kwa nyinyi, haimbidi yeye kupiga vita.

⁹⁶ Lakini ukiona huko kuunganishwa kwa nguvu za Mungu, zikikusanya kanisa Lake pamoja kutoka pembe nne za dunia, basi unaenda kuona jambo fulani likifanyika.

⁹⁷ Tunaona kwamba, katika siku za Sulemani, Mungu alimpa karama ya upambanuzi. Ilikuwa ni karama kubwa, karama ya kupambanua mawazo, na kadhalika, ya hekima. Na watu walikusanyika kuizunguka. Walimfanya kuwa mfalme. Na, unajua, yeye akawa ndiye mada ya kuongewa ulimwenguni. Kila mtu aliongea kuhusu Israeli. Sasa, hawakuwa na simu na televisheni, na vitu, wakati huo, walieneza habari kutoka mdomoni hadi sikioni. Na kila watu waliopitia wangeona karama hii kuu ya Mungu, ikifanya kazi, na watu wangeninii, mbona, wange—wangeambia kila mtu. Na umaarufu wake ukaenea ulimwenguni kote. Na wote hawakuwa na vita, hakuna shida, kwa sababu walikubali karama ambayo Mungu aliwapatia.

⁹⁸ Sisi sote, usiku wa leo, sisi Presbiteri, Methodisti, Baptisti, sehemu ya Pentekoste, tungeweza sote kutupilia mbali mawazo yetu, na kurudi na kuona kile ambacho Mungu alisema kuhusu Hiyo, na jinsi Yeye alivyosema Hiyo ilipaswa kutolewa. Hawezi kubadilisha Hiyo. Jinsi Hiyo ilivyoshuka kwenye Siku ya Pentekoste, hivyo ndivyo Hiyo ilivyoshuka katika nyumba ya Kornelio. Na kila wakati Hiyo ilipowahi kushuka, Hiyo ilishuka vile vile, chini ya maagizo yale yale ambayo Petro aliandika, katika Matendo. Na hivyo ndivyo yangali yamesimama. Hayana budi kubakia hivyo. Njia yoyote nyingine... Hapana mahali pengine katika Biblia ambapo waliwahi kupokea Hiyo kwa njia yoyote nyingine kuliko kutimiza yale maagizo ya Matendo 2.

Hiyo ni hakika. Hiyo ni, na sisi tunapata Hiyo leo hii, hivyo ndivyo haina budi kuja.

⁹⁹ Lakini katika unyoofu, mtu humpokea Mungu na kumwamini Yeye, lakini kama wangeninii tu...Halafu wanajivuta na kujitoa wenyewe, na “Hilo, sisi tuna *hili* na hayo ndiyo yote yaliyoko kwa Hilo.” Halafu wanajitenga wenyewe. Halafu hawatachukua ufunuo wowote mpya. Wanaliundia dhehebu. “Ndilo hili. Hili ndilo fundisho letu,” wanamalizia na ki-kituo. Kama ungekuwa na dhehebu ambalo litamaliza fundisho lenu na koma, “Tunaamini *hili*, pamoja na yote ambayo Mungu atatuonyesha,” basi hilo ni sawa, nitaenda hilo; bali si kwa kituo. Maana, Mungu ni Mungu, na wakati unasonga.

¹⁰⁰ Daima tunajaribu kutazama nyuma na kuona kile Moody alichosema, kile Sankey alichosema, kile Finney alichosema, kile Wesley alichosema, kile Luther alichosema. Hao walikuwa ni watu wa siku hiyo.

¹⁰¹ Sayansi haiangalii nyuma na kuona kile sayansi ilisema. Mbona, miaka mia tatu iliyopita, mwanasayansi Mfaransa alithibitisha kwamba ikiwa mtu angewahi kuenda kwa kasi ya kutisha ya maili thelathini kwa saa moja, uvutano ungemwondoa ardhini. Ungeweza kuwazia sayansi ya kisasa ikisema hilo? Leo hii anaenda karibu maili elfu mbili kwa saa moja, akijaribu kupata kitu cha kuzuia kuyeyuka kwa chuma ili aweze kuenda maili elfu nne kwa saa moja. Hawaangalii nyuma na kumreja huyo. Wanatazama mbele.

¹⁰² Bali kanisa daima linaangalia nyuma. Hebu tutazame juu! Kwa kuwa, nguvu zao zina kikomo. Na sisi tuna nguvu zisizo na kikomo, “Kwani mambo yote yanawezekana kwao wanaomwamini Mungu.” Imani halisi ya kweli itaitikia kila Neno ambalo Mungu ametoa, kwa “amina.” Sio, “Vema, lilikuwa kwa ajili ya kizazi kingine.” Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele!

¹⁰³ Sasa tunaona kwamba Sulemani, habari zilienea sehemu kubwa sana hata zikaenda kote hata huko chini kuingia Sheba. Na wao walikuwa na malkia huko chini, hapana shaka alikuwa ni maskini mama mzuri. Angewatawala watu wake. Na, unajua, walianza kumwambia kwamba kulikuwa na Mu—Mungu mkuu huko juu Israeli, na Yeye alikuwa amemtia upako mwanadamu kwa karama ya upambanuzi aliyekuwa ni mtu mkuu, hata hakuna mwanadamu angeweza kuwa na hekima kama hiyo. Ilibidi itoke kwa mungu fulani. Na, unajua, “Imani huja kwa kusikia, kusikia Neno.” Na ilichoma moyo wake, kama ilivyofanya maskini yule mwanamke asiye mwadilifu kwenye kisima jana usiku. Ilichoma moyo wake, na akaanza kutamani kujua kuhusu hili.

¹⁰⁴ Nafikiri inampasa yeyote wetu, tukipata kujua mahali Uzima wa Milele ulipo, maana tunajaribu kuishi.

105 Vema, kila msafara ulipitia, labda angesimama na kuwaleta katika ikulu. “Je! mlipitia Palestina?”

106 “Naam, tuna manukato fulani, na mapambo na vitu kutoka huko.”

“Vema, je! ni kweli kuhusu ile karama kuu ya Mungu wao?”

107 “Ni kweli. Niliiona ikifanya kazi.” Unaona, imani huja kwa kusikia.

108 Ndipo basi akaanza, akaanza kuona kiu. Alitaka kuona, mwenyewe.

109 Sasa alikuwa na magumu mengi ya kupitia. Kitu cha kwanza, yeye alikuwa ni kafiri. Kitu kingine, yeye alikuwa ni malkia. Na hapana shaka, kufanya hili, ingembidi kwenda kwa kuhani wake mwenyewe, kupata idhini kuenda huko juu kusikia hili. Kwa hiyo ninaweza kuwazia. . . Kama nikisikika wa kukufuru, simaanishi hili sasa. Ninaenda tu kuwapatia mchezo mdogo wa kuigiza hapa. Ninaweza kumwazia akienda huko chini kwa kuhani, na kusema, “Baba mtakatifu?”

“Naam, binti yangu,” kasema kuhani.

110 “Nimekuwa nikisikia habari kwamba huko juu Israeli wanaye Mungu huko juu, ambaye amemtia upako mwanadamu kwa upambanuzi Wake Mwenyewe na nguvu.”

111 “Sasa sikiliza, binti yangu. Kama, kama miungu mikuu ingeanzisha uamsho, ungekuja miongoni mwetu.” Unajua, haiwabidi wote kuwa makuhani wa kikafiri, kuamini hilo. Unaona? “Kama wangeanza uamsho kamwe, wangepanya chochote katika shirika letu. Wasingekuwa miongoni mwa hao wengine, unaona. Hata hivyo, wao ni kundi la watakatifu wanaojibingirisha.” Vema, sikutaka kusema hilo, unaona, lakini unajua. “Wao—wao—wao, wao si kitu. Hilo ni kundi tu la mashupavu wa dini. Wanasimulia kila namna za hadithi kuhusu kuvuka Bahari ya Shamu, ambazo si kitu ila hekaya. Kwa hiyo huwezi kuliadini kundi hilo huko juu, kwa sababu wao ni—wao ni kundi tu la siasa kali. Sasa ikiwa kuna nguvu zozote, ziko katika mungu mkuu, Dagoni, au baadhi ya hawa hapa.”

112 Ninaweza kumsikia maskini mwanamke huyo, alizungumza kwa dakika moja, akasema, “Lakini, unajua, wananiambia kwamba Mungu huyu waliye naye huko juu ni Mungu halisi.”

“Mbona,” akasema, “binti yangu, *huyo ni* mungu halisi.”

“Lakini, wao, wananiambia kwamba Mungu huyu huko juu ana uhai.”

113 Unaona, wakati—wakati—wakati kitu fulani kwa kweli kinashika moyoni, Mungu atazungumza na wewe kama utaendelea tu kuongea. Unaona, “Usiwazie kile utakachosema; utapewa hicho katika saa hiyo.”

¹¹⁴ Ndipo kasema, “Wanasema Mungu huyu hapa juu ni Mungu ambaye anawapenda watu Wake, ndipo Yeye anashuka chini na Yeye anajifanya Mwenyewe ajulikane kupitia watu Wake.”

“Ah, hakuna kitu kwa hilo. Sikiza.”

Loo, unasema nini? “Sasa kidogo tu. Ninapanda juu.”

¹¹⁵ “Ukienda huko juu, wewe, mbona, utaleta fedheha. Usihudhurie uamsho huo. Kwa sababu, hatushirikiani, unajua, kwa hiyo hupaswi kufanya hivyo.” Unaona?

¹¹⁶ “Pia unajua,” malkia akasema, yeye akasema, “mama wa nyanya yangu alitumikia hicho kinyago, hiyo sanamu, ama nyanya yangu na mama yangu, watu wangu wote walizitumikia hizo sanamu, na hukujawa na mojawapo iliyoonyesha chembe yoyote ya uhai. Ni ninii tu... Sijali ni magombo mangapi unayoweza kusoma, na chochote zaidi, hazijaonyesha chembe yoyote ya uhai. Na wao wanasema, ‘Huu ni Uzima.’ Na hii ni... Nina shauku kuhusu hilo.”

¹¹⁷ Vema, ninaweza kumsikia akisema, “Sasa, tazama, ukienda huko juu, ninaenda kulazimika kukutenga. Ninaenda kuchukua ninii yako... Wewe ni mshiriki mwanzilishi hapa, unajua. Na kama mimi... Na wewe una hadhi fulani, na wewe utashusha hadhi yako ukienda miongoni mwa kundi kama hilo.” Unaona?

“Vema, acha iwe hadhi, au sivyo!”

¹¹⁸ Unajua, wakati Mungu akianza kushika moyoni mwa mtu, hakuna kitu kinachoenda kusimama njiani mwao. Wanaenda kufika huko, hata hivyo, na Mungu anaenda kuhakikisha; sijali kama ni mume, mke, mtoto, mhubiri, mchungaji, yeyote yule, wakati njaa ikija kwa ajili ya Mungu.

¹¹⁹ Sasa tunamwona maskini mama huyu, wakati alipokuwa tayari, alisema, “Vema, mimi—mimi ninaenda, kwa vyovyote vile.”

¹²⁰ “Lakini tutakutenga. Jina lako halitakuwa hapa.”

“Vema, afadhali uliondoe tu, kwa sababu mimi ninaenda.”

¹²¹ Kwa hiyo sasa basi, ilimbidi kulipa gharama. Wengi sana wetu hawataki kulipa gharama. Afadhali tushikilie kanuni fulani ya imani.

¹²² Sasa, mwanamke huyo hapana shaka alikuwa ameyasoma magombo ya dini hii. Alikuwa ameona kwamba hiyo ilikuwa ni tabia ya Mungu; na kwamba Mungu, Mungu mwenye hekima yote, alimpa karama mwanadamu, kwamba Mungu Mwenyewe alikuwa akijidhihirisha Mwenyewe, si kupitia sanamu bubu, bali kupitia mwanadamu.

¹²³ Jinsi ambavyo upagani ni mfano mkamilifu, ama, ninii... ama, mfano wa Ukristo, jinsi ambavyo mwabuduo wa kikafiri ataanguka mbele za sanamu na kusujudia mwenyewe, katika

njia, kwamba yeye—yeye anaamini kwamba sanamu hiyo huzungumza na kumjibu.

124 Kama M—M—Mhindi wa Navaho. Walikuwa na kasha kwa ajili ya mungu wa mvua, akiwa na tope mgongoni mwake, na walimfanya huyo kuwa sanamu. Na kutengeneza gamba tupu, na wangeita, na wangesikia sauti yao wenyewe ikitoa mwangwi, na wao wakafikiria huyo alikuwa ni mungu wa mvua akiwajibu.

125 Ni tofauti jinsi gani ilivyo kwa Ukristo, hata hivyo. Tunasujudia wenyewe mbele za Mungu wa mbinguni ambaye si sanamu, na tunajazwa na Yeye na kuwa sanamu Yake, sura Yake iliyo hai ya Yeye, ikifanya kazi, ikitembea juu ya nchi kama wakilisho hai la Mungu yule tunayemtumikia. Mungu ndani ya mwanadamu! Ni kinyume na ukafiri; wanaangukia mbele za Mariamu fulani au Yusufu, ama mtakatifu fulani, au kitu kingine chochote kama hicho, ambacho kimekuwa mfu kwa miaka. Na, bali, unaona, Roho Mtakatifu huja ndani ya kiumbe hai, si ndani ya sanamu iliyokufa; bali ndani ya kiumbe hai, na hufanya kazi kupitia kiumbe hicho hai, si kupitia sanamu. “Nyinyi ndio mahekalu ya Mungu.” Unaona?

126 Kwa hiyo tunaona kwamba Mungu habadiliki, Yeye hufanya jambo lile lile usiku wa leo kama Yeye alivyokuwa akifanya katika siku za Sulemani. Alimpa Sulemani karama hii.

127 Na sisi tunaona, sasa maskini mwanamke huyu hana budi kujiweka tayari. Sasa, alikuwa na mambo mengi yakimkabili. Alikuwa na hali nyingi na vizuizi vingi, bali si imani yake. Imani yake haikuwa na chochote.

128 Sasa aliwazia hili, “Ninaenda huko juu. Na kama nikienda, na ikiwa kitu hicho ni sahihi, ninaenda kukiunga mkono. Kama si sahihi, ninaweza kurudisha zawadi zangu nyumbani.”

129 Unajua, anapaswa kuzungumzia baadhi ya watu wa Kipentekoste. Hiyo ni kweli. A-ha. Hiyo ni kweli. Unaenda hapa nje na kujiita mwenyewe Mpentekoste, na kuunga mkono vipindi vya redio ambavyo vinadhihaki kitu ambacho unaamini? Na hicho kiko miongoni mwa watu wako wenyewe, kusaidia kuunga mkono mpango wa Mungu. Unaona?

130 Sasa, lakini yeye alichukua fedha, dhahabu na manemane, na kadhalika, na akapakia ngamia.

131 Sasa, kitu kingine, alikuwa na sa—safari yenye hatari. Kumbuka, watoto wa Ishmaeli walikuwa jangwani, na wao walikuwa wanyang’anyi. Na jinsi ilivyo rahisi kwa kundi hilo la wanyang’anyi kumvamia maskini malkia huyu, pamoja na matoashi wachache alioandamana nao kama walinzi, na kuwaua hao na kuchukua hazina hii yote.

132 Lakini, unajua, wakati unapoona njaa na kiu kwa ajili ya Mungu, huoni hatari yoyote, huoni chochote. Unajaribu

kumfikia Mungu, na Mungu daima huhakikisha kwamba umefika huko.

¹³³ Alitaka kufika huko. Hiyo ndiyo shauku ya moyo wake, kwa hiyo Mungu alikuwa anaenda kuhakikisha kuwa amefika huko. Sasa, hakufikiria kuhusu hatari.

¹³⁴ Hufikirii kuhusu hatari. Hufikirii kuhusu ukosoaji. Hujali kile mtu mwingine asemacho. Ikiwa moyo wako una njaa sana kwa ajili ya Mungu, kusudi pekee ulilo nalo ni kumfikia Yeye. Haileti tofauti yoyote jinsi utakavyofika huko. Fika tu huko! Sasa, alikuwa na kusudi lilo hilo.

¹³⁵ Na sasa, hapana shaka, alichukua magombo yote na alikuwa anasoma, alipokuwa anaenda. Hapana shaka walisafiri usiku, kwa sababu, Jangwa hilo la Sahara, miale hiyo ya moja kwa moja ya joto ni joto sana, sana.

¹³⁶ Sasa wazia tu, alikuwa na umbali kiasi gani iliyombidi kusafiri, kuona hekima ya Sulemani. Ukipima kwenye ramani yako, ni mbali kabisa huko chini, yapata maili mia tatu. Na unajua ni muda gani uliomchukua? Sasa, hokusafiria Kadilaki iliyoyoyozwa, bali alienda juu ya mgongo wa ngamia. Na ilimchukua siku tisini, miezi mitatu, kufika huko.

¹³⁷ Si ajabu Yesu alisema, “Atasimama na kizazi hiki na kukihukumu kuwa kimekosa.” Baadhi ya watu wanaishi ng’ambo ya barabara, hata hawatatembelea mahali ambapo kitu hicho hicho kinaendelea. Hiyo ni kweli. Amina. Si ajabu yeye atasimama katika Hukumu pamoja na kizazi hicho sasa, na kukihukumu kwamba kimekosa. La, huku tukiwa na Makadilaki yaliyoyoyozwa, na magari ya moshi na ndege, na kila njia, Mungu aliiweka tu moja kwa moja mikononi mwako na tungali hatutafanya hivyo. Na yeye alikuja umbali huo wote kusikia hekima ya Sulemani, na hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani, Bwana Mungu Mwenyewe! Angalia!

¹³⁸ Ndipo tunapata ya kwamba alianza kupitia jangwani, akiyasoma hayo magombo, hatimaye alikaza mwendo mpaka akafika kule.

¹³⁹ Labda aliingia uani, uga wa ikulu au popote palipokuwa, na kupiga mahema yake, ambalo lilikuwa kawaida katika siku hizo, akiwa pamoja na wajakazi wake na matoashi wake, wakatulia.

¹⁴⁰ Na halafu hebu tuwazie tu, asubuhi iliyofuata, kengele ililia na—na tarumbeta zote zikalia, uimbaji ukaendelea, naye akaingia ndani na kupata kiti huko nyuma kabisa. Alikuwa kuona kwamba ni kitu gani, kweli au si kweli. Alitaka kujionea mwenyewe. Hakuwa tayari kuketi mbali huko chini. Kama alisikia kitu hiki mashuhuri, asingechukua kile alichosema mtu mwingine kukihusu. Alitaka kujionea mwenyewe.

¹⁴¹ Kama Filipino alivyomwambia Nathanaeli, katika somo letu jana usiku, kasema, “Laweza neno lolote jema kutoka Nazareti?”

Au kutoka...Nitakumbuka mahali hapo kwa dakika moja, mahali Yeye alipotoka. Kasema, “Laweza lolote jema kutoka Nazareti?”

¹⁴² Kasema, “Njoo uone. Usikae hapo na kukosoa. Njoo, ujionee mwenyewe.”

¹⁴³ Laiti tungeweza tu kufanya jambo lilo hilo usiku wa leo. Njoo, uone! Ichukue Biblia yako, chunguza kile unachoona kikiendelea. “Yachunguzeni Maandiko,” Yesu alisema, “kwani Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi.” Yeye ni Neno. Nayo Maandiko Yeneyewe ndiyo Neno, kwa hiyo Hilo humshuhudia Yeye wakati Maandiko yanapofanyika Uzima kwako, wakati Hilo limedhihirishwa ndani yako.

¹⁴⁴ Sasa tunaona kwamba yeye alikuwa amesoma magombo, na alijua tabia ya kile Yehova alichokuwa: hekima yote. Basi alipoyapiga mahema yake madogo, akaweka zawadi zake huko nyuma kwenye kona, kuona kama ilikuwa sahihi au la. Kama ni sahihi, inastahili kila kitu alichu nacho. Kama si sahihi, kirudishe.

¹⁴⁵ Nami nafikiri jambo lilo hilo usiku wa leo. Ikiwa mpango huu wa wokovu ambao tunapigania ni sahihi, tunawiwa kila kitu tulicho nacho, maisha yetu, muda wetu, kila kitu kingine chetu. Kama si sahihi, basi tafuta kilicho sahihi; maana unao tu uhai huu mmoja, na karibuni utaisha. Yachunguze Maandiko, kwanza, na uone kama yanaendana na Maandiko.

¹⁴⁶ Halafu tunamwona maskini mwanamke huyu akichukua kiti chake nyuma kabisa huko nyuma, kama wageni wote wanavyojaribu kufanya wakati mwingine. Ndipo baada ya tarumbeta kupigwa. Mchungaji Sulemani aliingia ndani, akaketi chini. Mkutano ukaanza. Kadi za maombi zikaitwa. Hilo linasikika kuwa baya, ila ninajaribu kujenga hoja. Naye akajua sasa. Akasema, “Nitaona mahali hekima hii ilipo.” Kwa hiyo mgonjwa wa kwanza, hatimaye ilifika, ama lolote swali lilikuwa, lilipokuja mbele za Sulemani, alilifunua. Akasema, “Labda, hiyo ni kweli.”

¹⁴⁷ Sasa, yeye hakutaka kusema, “Unajua, mtu huyo ana mawasiliano ya kimawazo, ninaamini.” Moyo wake ukaanza kuona njaa. Alianza kuamini, siku baada ya siku.

¹⁴⁸ Hatimaye iliwadia wakati wake kusimama mbele zake. Alikuwa na siri fulani, pia. Ndipo wakati alipokuja mbele za Sulemani, Biblia ilisema, kwamba, “Hakukuwa na kitu moyoni mwake kilichositirika kwa Sulemani.” Alifunua kila siri moyoni mwake.

¹⁴⁹ Ndipo wakati ilipofanywa juu yake, yeye alisimama kama kafiri mbele ya watu hao, na yeye akasema, “Yote niliyosikia ni kweli, na zaidi.” Akasema, “Heri watu wale waliopo hapa kuona kitu hiki kikiendelea kila siku.” Amina. Loo, ha—hakuwa na pumzi zaidi ndani yake, karibu. Wakati alipoona kwamba

wengine walifanyiwa hilo juu yao, na yeye akafanyiwa juu yake, na akamwamini Mungu.

¹⁵⁰ Si ajabu, si ajabu kwamba Yesu alisema kwamba, “Atasimama pamoja na kizazi hiki.” Wakati, hapo Yeye alikuwa amesimama hapo, akifanya jambo lile lile, ila tu kwa wingi zaidi, na ishara zenye nguvu zaidi; na wao walikuwa wamesimama hapo, “Onyesha,” wakisema, “tuonyeshe ishara kutoka Mbinguni.” Loo, jinsi watu wawezavyo kuwa vipofu! Alisema, “Yeye atasimama kwenye Hukumu, pamoja na kizazi hiki, na kukihukumu kuwa kimekosa.”

¹⁵¹ Na halafu baada ya miaka elfu mbili ya kuhubiri Injili, na Roho Mtakatifu akimwagika katika siku hizi za mwisho, juu ya watu, karama za Roho Mtakatifu, na kuahidi kwamba upambanuzi huu mkubwa ungerudi kanisani tena; angefanya nini kwa kizazi hiki wakati akisimama pale, baada ya wakati wake ukiongezea miaka elfu mbili ya kuhubiri Injili, katika siku hizi za mwisho kuona karama, si karama moja, bali karama za Roho Mtakatifu? Alisalimisha maisha yake kwa Kristo. Kwa nini?

¹⁵² Inanibidi kufunga, maana sininii... Ninataka—ninataka kuwaombea.

Marafiki, mnaona, walisema, “Tuonyeshe ishara. Tunataka...”

¹⁵³ Hiyo ndiyo shida ya Wapentekoste. Unatazamia kitu fulani, na moja ya siku hizi inaenda kuwa mbali sana. Ilipita moja kwa moja karibu nawe, na wewe hukujua.

Kumbuka, katika siku za Eliya, hawakumjua.

¹⁵⁴ Katika siku za Yohana Mbatizaji, hawakumjua. Na alinenwa habari zake, katika Maandiko, kwamba angekuwepo, “Ninamtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu, kutengeneza njia.”

¹⁵⁵ Na hata wanafunzi walikuja Kwake, kasema, “Ni kwa nini Eliya lazima aje?”

Yeye akasema, “Amekuja tayari, na nyinyi hamkujua hilo.”

¹⁵⁶ Hawakujua Yesu alikuwa ndiye Kristo, mpaka Yeye alipokufa na kuzikwa.

Hawakujua kwamba Ireneo alikuwa ni wa ninii ama...

¹⁵⁷ Nitasema hili, ili watu wote wajue. Hawakujua Joan wa Arc alikuwa ni mtakatifu wa Mungu, mpaka walipomwua. Kanisa Katoliki lilimchoma moto Joan wa Arc, kuwa ni mchawi, kwa sababu aliona maono na kuwaombea wagonjwa, akawafufua wafu. Na kanisa Katoliki likamwita mchawi, na kumchoma moto mwanamke huyo akifungwa kwenye nguzo. Ndipo yapata miaka mia mbili baadaye, walianka na kugundua kwamba alikuwa ni mtakatifu. Bila shaka, walifanya kitubio kikubwa,

walifukua miili ya hao makasisi na kuitupa kwenye mto. Upuuzi!

¹⁵⁸ Lakini kuwa mwangalifu, huenda likatendeka miongoni mwetu, kwamba kitu hicho huenda kikaja na kutambulishwa wazi na Mungu katika Maandiko, na kwa sayansi na kila kitu kingine, na kingetupita na tusijue. Halafu kisimame katika siku ya mwisho, kimetambulishwa wazi.

¹⁵⁹ Mwanadamu angali ni yule yule. Mwanadamu daima anamsifu Mungu kwa kile ambacho Yeye amefanya tayari, na wanazungumza kuhusu kile Yeye atakachofanya, na kupuuzia kile Yeye anachofanya. Hiyo ndiyo tabia ya mwanadamu.

¹⁶⁰ Hebu tumtazame Yeye, kile Yeye anachofanya sasa. Yeye ni Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele, Yehova Mungu yeye yule aliyedhihirishwa ndani Yake. “Katika siku hiyo mtajua ya kwamba Mimi nilikuwa ndani ya Baba, na Baba ndani Yangu; Mimi ndani yenu, na nyinyi ndani Yangu.” Mungu akiteremka kutoka kwenye Nguzo ya Moto, kuwa Mtu; na kutoka kwa maisha yaliyotolewa sadaka ya Mtu huyo, Damu iliyotusafisha na kushuka kuingia ndani yetu, kufanya ushirika tena, kuvuta na kutoa kanisa kwa ajili ya Edeni tena.

¹⁶¹ Kwa nini? Sasa kimya kwa dakika moja tu. Ni nini kilifanya hiki kwa yule mwanamke? Yeye alikuwa ni mtu anayekiri kuwa wa kidini, bali moyo wake ulikuwa unaona njaa kwa ajili ya kitu halisi. Alitaka kitu halisi.

¹⁶² Ikiwa unaona njaa kuona kitu fulani halisi, Mungu atakuonyesha. Daima utapata kile unachotafuta.

¹⁶³ Inanikumbusha, kama vile nyinyi watu wote mnajua kwamba mimi...nilikuwa nikizungumza na rafiki yangu hapa nyuma, Ndugu Brown, kitambo kidogo kilichopita. Ninakumbuka Dada Brown yupo hapa mahali fulani, alisema; abarikiwe. Jinsi nilivyoishi na hao watu huko chini katika siku zile za kwanza za huduma yangu! Na Ndugu Brown ni kama ndugu yangu kabisa, maana anapenda kuwinda. Dada Brown alimnunulia bunduki mpya ya marisaa ya atomatiki aina ya Browning. Nilimwuliza kama angali alikuwa nayo. Akasema, “Naam.” Ninaenda kumbadilisha kuwa bunduki, moja ya siku hizi, aachane na kitu hicho cha kale kinachotatarika.

¹⁶⁴ Sasa angalia. Lakini katika kuwinda, nilikuwa nikienda katika misitu ya kaskazini kuwinda kulungu, huko juu, New Hampshire na Maine, na ni makazi ya kulungu mwenye mkia mweupe. Na nilikuwa na mwenzangu huko juu, niliwinda naye. Na yeye alikuwa mwindaji mzuri, yapata robo damu ya Mhindi. Na haikukubidi kuwa na wasiwasi juu yake; huendi kumpoteza, anajua mahali pa kuenda. Na yeye alikuwa ni mwindaji hodari. Tungetengana, na mahali tungekutana juu ya milima myeupe na misitu mikubwa, lakini tungepatana. Na sisi hatukuwa wafuata nyayo; tuliwinda. Nilipenda kuwinda na Bert.

¹⁶⁵ Alikuwa ni mwindaji hodari, lakini alikuwa ndiye mtu mbaya kuliko wote niliowahi kuona. Mtu huyo alikuwa na moyo ndani yake kama jiwe. Alikuwa katili. Alikuwa na macho yaliyoonekana kama mjiusi, na yeye—yeye—yeye alikuwa tu mbaya, mbaya tu kabisa. Na alizoea kupenda kuwapiga risasi kulungu wadogo, hao ni watoto wa kulungu, ili tu kunifanya nisikie vibaya. Angewaua hawa kulungu wadogo, na mimi ningesema, “Bert, hivi huoni aibu kufanya hivyo?”

¹⁶⁶ Na yeye angesema, “Hivyo ndivyo tu ilivyo na nyinyi wahubiri, nyinyi ni waoga sana.”

Nikasema, “Bert, huo si woga. Huko ni kuwa katili.”

¹⁶⁷ Sasa, yote ni sawa, ji—ji—jinsia ya kulungu au ukubwa. Kama sheria ikisema unaweza kumwua mtoto wa kulungu, endelea umwue. Vema, Ibrahimu alimwua ndama na kumlisha Mungu. Hakukuwa na chochote kibaya na mtoto wa kulungu.

¹⁶⁸ Lakini kuwaua tu na kuwaacha wakae hapo, ili tu kuwa mbaya, hayo ni mauaji. Na mimi sipendi hilo, na ningemwambia. Ningesema, “Bert, wewe ni rafiki yangu, nami ninakupenda, na wewe ni mwindaji mzuri. Wewe ni mtu wa bunduki, mzuri wa shabaha, hodari wa shabaha.” Nikasema, “Ninakupenda, lakini—lakini wewe ni—wewe ni—wewe ni katili.”

¹⁶⁹ Na yeye angesema, “Loo, Billy, kama hukuwa mhubiri, ungekuwa mwindaji mzuri.”

¹⁷⁰ Ndipo nikasema, “Sikiza, Bert, unaweza kuwa na utu kuhusu hili.” Nikasema, “Hilo ni kosa.”

¹⁷¹ Akasema, “Wewe...” Nilikuwa bwana nyama kwa miaka, unajua. Na yeye akasema, “Wewe, ulikaa katika uhifadhi muda mrefu kupita kiasi.”

Nikasema, “La, sikukaa.”

¹⁷² Ndipo basi siku moja nilienda huko juu kuwinda. Ilikuwa ni karibu mwisho wa msimu. Nilikuwa nikifanya mikutano fulani. Na theluji ilikuwa imeshuka, yapata inchi sita, theluji nzuri ya kufuatia. Nami nikakutana na Bert, na yeye akasema, “Sema, Billy, ninacho kitu kipya kwa ajili yako.”

Nami nikasema, “Kitu gani?”

¹⁷³ Akachomoa kutoka kwenye shati lake filimbi ndogo, na akapuliza filimbi hii ndogo. Na ikasikika kama mtoto mchanga wa kulungu akiitia mama yake, unajua, mtoto tu mchanga wa kulungu, ule mlio mdogo wanaotoa.

¹⁷⁴ Ndipo nikasema, “Bert, humaanishi kuniambia kwamba wewe unge—ungefanya hivyo?”

Akasema, “Loo, jirudie, mhubiri.”

¹⁷⁵ Kwa hiyo siku iliyofuata tulienda kuwinda. Na kwa kawaida huwa tunabeba sandwichi, na—na kubeba chupa ndogo ya—ya chokoleti moto, maana ina sukari ndani yake, unajua, na ilitutia

joto. Naam, huwa kunakuwa baridi sana huko juu, kwenye wakati huo wa mwaka. Kwa hiyo sisi. . .

¹⁷⁶ Msimu ulikuwa umewadia. Na—na wakati ukifyatua bunduki kadhaa, unanena kuhusu Houdini kuwa bingwa wa kuchomoka, yeye alikuwa mwanafunzi kwa hao kulungu. Maana, wangetoroka mara moja sasa, waingie chini ya lundo la vichaka au chochote, na halafu wafanye malisho usiku kama mwezi unaangaza. Ndipo, kama hawakula, wangekaa na njaa, kabla hawajatoka nje, maana walijua ilikuwa ni kifo kutoka huko nje. Na kwa hiyo msimu ulikuwa umewadia, watu walikuwa wamewinda kwa majuma kadhaa.

¹⁷⁷ Basi tulitembea asubuhi yote, na hata hatukuona mburuzo mmoja. Yapata wakati wa adhuhuri, alikuwa anatembea mbele yangu. Tulikuwa tunaenda juu kwenye kilele cha njia nyembamba mlimani, halafu tutengane na kurudi njia mbili tofauti, na kuja kwenye kambi usiku huo, labda tuingie saa tatu, saa nne. Kama tulimwua kulungu, tungemtundika juu, kusudi sote wawili turudi siku iliyofuata na kusaidia kumwingiza ndani. Kwa hiyo tulikuwa tunapanda juu, kutengana, na hatukuwa tumeenda juu ya eneo la msitu bado.

¹⁷⁸ Ndipo yapata saa tano u nusu au saa sita, Bert kwa namna fulani aliinama chini. Theluji ilikuwa inakuwa ya kilindi sana, juu kwenye mlima. Na kwa namna fulani aliinama chini, na nikafikiria alikuwa amefikia huko nyuma. . . Hakusema mengi sana. Na akafikia huko nyuma, nilifikiria alikuwa anaenda kuchukua chakula chake cha mchana; nami nikaenda kuchukua chakula changu cha mchana. Nikawaza, “Vema, tutakula. Hapa ndipo tunaachana, na yeye atazunguka upande *huu*, na mimi nitaenda njia nyingine.”

¹⁷⁹ Naye akaketi chini. Kulikuwa na mahali padogo palipo wazi, yapata ukubwa wa jengo hili mara mbili, maskini ninii tu, kile tunachokiita, maskini kitu kama bustani la nyasi. Hatukuwa tumeona mburuzo asubuhi yote. Ndipo akaketi chini kando ya hili, chini, karibu na miti fulani, kidogo kama hifadhi ndogo ya theluji; akainama chini namna *hii*, kana kwamba alikuwa anaenda kuchukua chu—chupa yake ya themosi au sandwichi yake, akaanza kuitoa. Nami nikafikia yangu. Ndipo akatoa filimbi hii ndogo. Na yeye akanitazama, kwa hayo macho ya mjiusi.

¹⁸⁰ Ndipo akaipuliza filimbi hii. Na wakati alipoipuliza filimbi hii, angeweza kuifanya ifanye kazi kweli, ilisikika tu kama mtoto wa kulungu. Basi wakati alipofanya hivyo, kwa mshangao wangu, moja kwa moja upande wa pili wa mahali hapo palipo wazi, mama mnene mkubwa wa kulungu alisimama. Huyu ni kulungu wa kike, jike; mnyama wa kupendeza, macho makubwa ya hudhurungi, na hayo masikio yamesimama. Ndipo akanitazama, namna *hiyo*, na namna ya tabasamu hilo la

kipumbavu. Akanitazama namna hiyo, akarudisha filimbi yake. Nikawaza, “Bert, hutafanya hilo.”

¹⁸¹ Akasema, “Sh.” Na mimi nikaona. . . Aliipuliza tena, kidogo kabisa, kwa wepesi.

¹⁸² Na, sasa, hilo si kawaida kwa huyo kulungu. Wakati huo wa mchana, saa tano mchana, kutoka nje? La. Ilikuwa ni kitu gani? Mtoto wake alikuwa katika shida. Alisimama. Nilimtazama, nyuma ya kichaka hiki.

¹⁸³ Ndipo akaipuliza tena. Huyo kulungu akapiga hatua mbili au tatu mbele, akija moja kwa moja hadharani.

¹⁸⁴ Hilo kabisa si kawaida. Naam, bwana, asingefanya hivyo. La, bwana. Bali ilikuwa ni nini? Mtoto wake alikuwa katika shida.

¹⁸⁵ Na yeye akatembea hatua chache zaidi, hayo masikio makubwa, akageuka upande. Ndipo maskini Bert akanitazama. Na nikawaza, “Ah-loo.” Nilimwona akiweka hiyo risasi kwenye mtutu wa hiyo thelathini-sufuri-sita, na kuteremsha chini huo wenzu.

¹⁸⁶ Akasimama, na hiyo shabaha ya darubini hiyo ikaja moja kwa moja kupitia moyo wake. Basi wakati yeye alipoinua bunduki yake, kulungu huyo akamwona mwindaji. Akageuka.

Naye akapuliza filimbi hiyo tena.

¹⁸⁷ Unajua, kwa kawaida huyo kulungu angekuwa ametoroka. Bali si yeye. Kwa nini? Alikuwa mama. Hakuwa anajifanya chochote. Ndani yake, alizaliwa mama. Mtoto wake mchanga alikuwa katika shida. Ingawa alijua ingemgharimu maisha yake, hakujali. Alikuwa mama. Hakuwa anafanya namna fulani ya maigizo. Ilikuwa halisi, maisha yake. Alikuwa mama.

¹⁸⁸ Ndipo nikamwona mwindaji akituta bunduki yake; naye alikuwa hodari wa shabaha. Nami nikageuza kichwa changu. Nisingeweza kutazama hiyo. Nikawaza, “Mtu huyo katili awezaje kulipua moyo huo mtiifu wenye thamani unaodunda kwa ajili ya mtoto wake mchanga? Anawezaje kulipua moyo wake kutoka kwake?” Na mimi nilijua kwamba risasi hiyo kubwa kama uyoga ya mia moja-na-themanini ingelipua moyo wake kabisa kupita kwake, katika masafa hayo. Nikawaza, “Anawezaje kupanya hilo?” Ndipo nikageuza mgongo wangu, kujiepusha na kuona hilo.

¹⁸⁹ Ndipo nikaanza kuomba. Nikasema, “Baba wa Mbinguni, mtu huyo anawezaje kuwa katili hivyo? Huyo mama wa thamani, hawezi kusaidia hilo. Hafanyi maonyesho. Yeye yu halisi. Na yeye ni—na yeye ni mama, na ameitwa, akijaribu kumtafuta mtoto wake. Hata ikigharimu maisha yake, mtoto wake yuko taabuni.” Na mimi nilikuwa nikiomba, kwa nafsi yangu, nikisikiliza katika wakati wowote kusikia hiyo nyundo ikifyatuka, kuanguka, na hiyo bunduki kulipuka. Na mimi nilikuwa tu nimesimama hapo nimejishika namna *hii*, nikiomba.

¹⁹⁰ Nikangoja, nikangoja. Bunduki haikufyatuka. Nikangoja tu kidogo. Ndipo nikageuka kuangalia, na yeye alikuwa anaenda *hivi*. Hakuweza kushikilia bunduki itulie. Nikamwangalia kote.

¹⁹¹ Akanitazama. Mtazamo wake ulibadilika. Hayo macho ya mjusi yalikuwa yameshuka kuwa kitu kingine. Machozi yalikuwa yanatiririka mashavuni mwake. Akatupa bunduki chini. Akasema, “Billy, yamenitosha. Niongoze kwa huyo Yesu unayenena habari zake.”

¹⁹² Hapo kwenye lundo hilo la theluji, alasiri hiyo, nilimwongoza mtu huyo katili kwa Yesu Kristo. Kwa nini? Kwa sababu aliona kitu halisi, kitu ambacho hakikuwa ni kujifanya, kitu ambacho kilikuwa halisi.

¹⁹³ Loo, ulimwengu huu wenye njaa unatafuta kitu halisi, kitu ambacho si kujifanya, kitu ambacho ni cha kweli, kilichozaliwa na Mungu, kinachotoka kwenye Biblia. Je! wewe, alasiri ya leo, mama, ndugu; hivi wewe, Mkristo, usingetaka kuwa na Yesu Kristo sana moyoni mwako, wingi wa Roho wa Mungu ndani ya moyo wako, ambaye angekusukuma kufanya mambo maaminifu kama yule kulungu alivyomfanya mtoto wake? Je! hungetaka kuwa Mkristo wa namna hiyo? Je! ungetaka kuwa na wokovu wa namna hiyo ambao... wewe... kifo au chochote kingine, na u—upendo tu wa Mungu moyoni mwako, kama yeye alivyokuwa na upendo wa mtoto wake?

¹⁹⁴ Sasa njia ya pekee inayoweza kuwa. Huwezi kufanya hivyo kwa kujiunga na kanisa. Huwezi kufanya hilo kwa kuweka jina lako kwenye kitabu. Haina budi kuwa halisi. Haina budi kuwa cha kweli. Haina budi kuwa ni kuzaliwa. Haina budi kukubadilisha, kutoka kwa imani tu ya kujifanya, kuwa Mkristo halisi.

¹⁹⁵ Ulisema, “Je! unafikiri upendo ungekuwa mkuu namna hiyo? Je! unafikiri Yeye angeweza kunipenda?”

¹⁹⁶ Akasema, “Mama anaweza kusahau mtoto wake anayenyonya, bali Mimi siwezi kuwasahau. Majina yenu yamechorwa kwenye vitanga vya mkono Wangu.”

¹⁹⁷ Mungu alikuja duniani, katika umbo la Mwanadamu, na—na—na kujifunua Mwenyewe, akasimika hema Lake; kutoka kuwa Yehova Mungu, kuwa Mwanadamu, kustahimili aibu na laana. Mtoto Yehova Mungu katika hori, chini ya lundo la samadi, huko chini akilia katika hori; Mungu, Muumba wa Mbingu na nchi, akisimama pale katika mwili wa binadamu, kuchukua kifo cha dhambi zako juu Yake Mwenyewe, kusudi Yeye aweze kukuweka huru kuwa Mkristo zaidi kuliko vile yule kulungu alivyokuwa mama. Unawezaje kukataa upendo kama huo usio na kifani? Halafu, mbali na huo, Yeye aliandika Neno Lake. Hilo latosha. Usingeweza kuchukua neno langu, inakubidi ku... ingekuwa sawa, bali si Yeye. Yeye alipaa Juu na kuwapa wanadamu vipawa. Alirudi katika umbo la Roho

Mtakatifu, Mungu yeye yule, kufungua moyo wako, kwa Damu ya upatanisho.

¹⁹⁸ “Iweni wakamilifu basi, kama Baba yenu Mbinguni pia alivyo mkamilifu.” Hakuna mmoja wetu awezaye kuwa hivyo. Siangalii kile nilicho mimi. Mimi, mimi sistahili. Wewe hustahili. Ni nani anayestahili? Siangalii kile nilicho mimi; ninaangalia kile alichu Yeye. Yeye Ndiye aliyeangaliwa. Yeye ni Sadaka yangu. Mimi sistahili kusimama hapa kama mhudumu. Kama nilihesabu kustahili kwangu, ninge—ningekuwa Kuzimu, na wewe pia. Lakini hatuungalii kile tulicho.

¹⁹⁹ Unasema, “Nisingeweza kufanya hilo. Nisingeita. Nisingegusa vazi la Mungu. Nisingefanya *hili*.”

²⁰⁰ Loo, unaweza! Ati kuangalia kilichotendeka? Yeye alikufa, ili kwamba uweze kufanya hilo, ili uweze kuokolewa. Hiyo ni ya kweli. Je! ungependa kuwa namna hiyo, na ungetaka kukumbukwa katika maombi? Inua mkono wako, useme, “Ningetaka, Ndugu Branham.”

Hebu tuinamishe vichwa vyetu.

²⁰¹ Huku tumeinamisha vichwa vyetu, njoni kwa utamu, kwa upole sasa. Hatuna nafasi hapa kwa ajili ya wito wa madhabahuni. Hata hakuna madhabahu. Lakini Biblia ilisema, “Wote walioamini, walibatizwa.” Wito wa madhabahuni, ulikuja katika siku ya Methodisti, ambao ni sawa. Lakini katika wakati wa Bwana wetu na mitume, wao “walamini kwa Uzima.” Mtu “uliokolewa kwa imani, kupitia neema.” Kama hujapata tukio hilo usiku wa leo, ndugu, dada!

²⁰² Wanawake, kama huna neema ya kutosha moyoni mwako, usiku wa leo, kujua kwamba Biblia inafundisha ya kwamba unapaswa kuacha kunyoa nywele zako, kuvaa kaptura na vipodozi! Kama huna neema kiasi hicho moyoni mwako, usiku wa leo! Na unajua Biblia inafundisha unapaswa kuwa nayo. Yeye hawezi kubadilika. Unasema, “Sivai kaptura. Ninavaa suruali fupi.” Hiyo ni mbaya zaidi.

²⁰³ Mungu alisema, “Mwanamke atakayevaa vazi limpasalo mwanaume, ni chukizo kwa Mungu.”

²⁰⁴ Na wewe mwanamume ambaye huwezi kuacha kunyosha shingo yako na kuwaangalia wanawake waliovalia kizinifu, sanamu za leo hii! Wewe mwanaume usiye na neema halisi ya kutosha moyoni mwako kumfanya mke wako na watoto kuacha kufanya mambo kama hayo, upendo wa Mungu haujatiwa nanga moyoni mwako; usiitwe mwana wa Mungu. Wewe ungali Sodoma, mwanaume ambaye hawezi kuitawala nyumba yake mwenyewe; Mungu alimkusudia kufanya.

²⁰⁵ Na enyi mashemasi mliooa mara mbili au tatu! Na enyi wanaume mnaokimbia nje kuacha wake zenu, na mnajaribu kushikilia maungamo yenu! Enyi wanawake mliovuka njia ile

nyingine! Nyinyi watu ambao hujificha nyuma ya joho la kanisa! Dhehebu lako halitakuwa na chochote kuhusiana na jamaa huyo mwingine, mwache awe Mkristo au sivyo; kama yeye si wa kundi lenu, hutakuwa na uhusiano wowote naye. Aibu kwako!

²⁰⁶ Naomba Mungu adhihirishe halisi, usiku wa leo, kwako wewe. Naomba uje Kwake, kwa utamu sasa, na useme, “Bwana, nisamehe dhambi zangu. Tangu usiku huu, na kuendelea, nitakutumikia Wewe.”

²⁰⁷ Nyinyi mnaopenda kipindi cha televisheni, ambao mtakaa nyumbani kumwona nyota fulani wa sinema mzinifu kama vile *Tunampenda Sucy* au vipi kuhusu upuuzi ule mwingine walio nao, kukaa nyumbani Jumatano usiku kutazama televisheni badala ya kuja kwenye chumba cha maombi, upendo wa Mungu umetoka moyoni mwako. Unafanya hayo, na ungali unashikilia uanachama wako? Upendo wa Mungu ungekusukuma kutoka kwa hayo, na kukusukuma kwenda katika kanisa lako, kwa ndu—ndugu yako na dada; kuja pamoja, kuketi katika mahali pa Mbinguni na kusikiliza mchungaji wenu akihubiri. Na u—uamsho, au kambi, inaisha sasa. Ikiwa hiyo ingali imebaki moyoni mwako, hebu tuombe pamoja sasa kwamba Mungu ataiondolea mbali.

²⁰⁸ Bwana Yesu, tunakuja na majuto manyenyekevu, tunakuja na mioyo yenye toba, Bwana. Sisi sote tuna hatia. Tumefanya kosa dhidi ya Amri Zako. Tumezivunja sheria za upendo Wako ambao ulituochoa. Kanisa lenyewe limeenda mbali katika misisimko na mipango ya ujenzi, na kila namna ya upuuzi; na kuacha mkutano wa maombi na—na Roho Mtakatifu kwa ajili ya kitu kingine mara moja au mbili kwa juma, wakati kinapaswa kuwa mioyoni mwetu na niani daima. Tusamehe, Bwana.

²⁰⁹ Wasamehe wahudumu wetu, Bwana, ambao watasimama mimbarani na kuona aibu kutangaza Injili yote ya Kristo. Jinsi ambavyo wengi wao leo hii. . . Ulimwengu wote umekuwa Sodoma. Wahudumu wengi wakiketi katika parokia yao, usiku wa leo na kesho, au katika chumba chao cha kusomea, wakijaribu kutafuta maneno; na kukumbana na Neno la Mungu, na kuona dhambi, lakini wanaogopa kusema chochote kuhusu hilo, kwa sababu wangetengwa. Halmashauri ya mashemasi litawaita, na watarudishwa kwenye makao makuu na kutolewa nje, huku wanajua wanapaswa kuhubiri dhidi ya dhambi. Ni Lutu, tena, “Dhambi za Sodoma ziliitesa nafsi yake yenye haki.” Lakini mtu hana ujasiri. Kama tu vile Lutu, hakuwa na ujasiri kusimama.

²¹⁰ Ninaomba, Mungu, Wewe utatusamehe mambo kama hayo. Jalia tuwe kama Paulo wa kale, “Sikujiepusha na kuwahubiria habari ya kusudi lote la Mungu.” Tusamehe sote, Baba.

²¹¹ Kama vile hadithi hii ndogo rahisi, ya ile siku ya Novemba yenye baridi, juu ya kilele cha mlima ule kule; jinsi ambavyo mtu

yule, usiku wa leo, shemasi kanisani kule juu, Mkristo mtiifu, kwa sababu mama kulungu alijitokeza na kudhihirisha kitu halisi. Ulisema, “Kama—kama wakinyamaza, miamba itapiga makelele.”

²¹² Ninaomba, Baba, kwamba Wewe utatupatia kitu halisi sana, usiku wa leo, ambacho kitavutia usikivu wetu kwa Kristo, kutufanya tujue kwamba Yeye yuko miongoni mwetu, usiku wa leo.

²¹³ Mikono ya toba iliinuliwa, mamia ya hiyo. Wasamehe, Bwana. Sasa ninakukumbusha Wewe, Bwana, juu ya Andiko ambalo Wewe ulisema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu isipokuwa Baba Yangu amvute kwanza.” Wangewezaje kuinua mikono yao isipokuwa Wewe uliwavuta? Wakati wakiinua mikono yao, wanavunja kila sheria ya kisayansi. Uvutano hushikilia mikono yao chini. Lakini kulikuwa na roho fulani ndani yao, na kwa Roho karibu nao, aliyesema, “Uko makosani. Inua mikono yako.” Na ilienda kinyume cha kanuni za uvutano, na kuinua mikono yao kumwelekea Muumba, “Nirehemu, Mungu.”

²¹⁴ Na Wewe ulisema, “Wote ambao Baba amenipa Mimi watakuja Kwangu. Sitawatupa nje kamwe. Nitawapatia Uzima wa Milele, na kuwafua katika siku ya mwisho.” Ulisema, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka Mimi, yuna Uzima wa Milele, wala hatakuja Hukumuni, bali tayari amepita toka mautini kuingia Uzimani.”

²¹⁵ [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...kwa Ufalme wa Mungu, kufanya washiriki watiifu wa Mwili wa Kristo. Na makanisa yao, ya wahudumu hawa, yaweze kukua na kukua na washiriki, waliozaliwa mara ya pili, katika Ufalme wa Mungu. Wabariki ndugu zangu, kwamba yeyote watakayemwombea aponywe; Injili wanayohubiri, isianguke kwenye udongo mgumu, wenye miamba, bali kwenye mioyo miororo.

²¹⁶ Tujalie, Bwana, kwamba Ufalme wa Mungu hivi punde utaimarishwa duniani. Unakuja kwa ajili ya majumbe Wako. Siku moja Mwana-kondoo anaenda kuondoka kwenye mahali patakatifu, aje kuchukua Kitabu kutoka mkononi Mwake Yeye aliye Mmiliki wa hatimiliki ya hicho. Wakati mwanadamu alipokosa, na Kitabu cha Uzima kikarudi kwa Mmiliki wake wa asili. Mwanadamu, uhai wote ulipotea; na hakukuwa na mtu, Mbinguni au duniani, aliyestahili. Bali Mwa—Mwana-kondoo alijitokeza, Mwana-kondoo aliyelowa Damu ambaye alikuwa amechinjwa tangu msingi wa ulimwengu, ambaye alikuja na kukitwaa Kitabu cha Ukombozi na kufungua Hicho. Mungu, naomba jina langu liwe humo. Jalia kila jina hapa liandikwe Humo, Bwana, ambalo limekombolewa katika mpango huu mkubwa wa ukombozi. Tujalie, Baba.

²¹⁷ Na sasa tunawatoa Kwako. Ninawakabidhi Kwako. Na iwapo kuna yeyote hapa ambaye hajawahi kubatizwa katika ubatizo wa Kikristo, naomba waje mbele, kwa tendo la imani, na kukiri kwamba wako makosani, wakabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zao, na kujazwa na Roho Mtakatifu. Tujalie, Baba.

²¹⁸ Naomba Wewe utusikie, Baba, katika maombi haya, tunapoyaleta Kwako kwa unyenyekevu, katika Jina, Jina lilitoshelezalo kwa yote ambalo Mbingu zote na nchi zinaitwa hilo, Yesu Kristo. Amina.

Kuna Chemichemi iliyojaa Damu,
Iliyotolewa kutoka kwenye mishipa ya
Imanueli,
Na wenye dhambi wakitumbukia chini ya
gharika hilo,
Hupoteza waa lao lote la dhambi.
Hupoteza waa lao lote la dhambi,
Hupoteza waa lao lote la dhambi;
Na wenye dhambi wakitumbukia chini ya
gharika hilo,
Hupoteza waa lao lote la dhambi.

²¹⁹ Hivi hamupendi nyimbo hizo za kale? Endelea. Hizo si ni za ajabu? Ziliandikwa na Roho Mtakatifu. Mimi ninazipenda tu. Nafikiri nyimbo za yubile ni nzuri, bali ninapenda nyimbo hizi za kale za Damu, nyimbo za Imani. Hebu tuuimbe, ubeti mwingine, mtindo wa kale, njia ya kishamba, jinsi tulivyouimba huko nyuma vilimani miaka iliyopita.

Mwivi anayekufa alifurahia kuona (nafasi
yake ya mwisho)
Chemichemi hiyo katika siku yake;
Hapo naomba mimi, ingawa ni mwovu kama
yeye,
Niliosha na kuondolea mbali dhambi zangu
zote.

²²⁰ Hebu tufumbe macho yetu na tumwimbie Kristo huo kwa utamu.

Mwivi anayekufa alifurahia kuona
Chemichemi hiyo katika siku yake;
Na hapo naomba mimi, ingawa ni mwovu
kama yeye,
Nioshe na kuondolea mbali dhambi zangu
zote.
Nioshe na kuondolea mbali dhambi zangu
zote,
Nioshe na kuondolea mbali dhambi zangu
zote;

Na hapo naomba mimi, ingawa ni mwovu
kama yeye,
Nioshe na kuondolea mbali dhambi zangu
zote.

221 Loo, hivi haukufanyi kujisikia kama umesuguliwa kabisa ndani, unahisi tu utamu wa Uwepo wa Mungu? “Sasa nyinyi ni wana wa Mungu. Sasa tumeinuliwa juu katika mahali pa Mbinguni ndani ya Kristo Yesu,” pamoja na mamlaka yote, tumepewa Mbingu na nchi. Je! mliwahi kuwazia hilo?

Mtu fulani anasema, “Je! una nguvu zozote?”

“La, bali ninayo mamlaka.”

222 Ni kama maskini polisi anayesimama hapa nje mtaani, jamaa mdogo mwenye kofia iliyovutwa juu ya masikio yake, uzito wake yapata ratili mia moja, beji ikiwa juu yake. Basi hapa linakuja lundo la motokaa chini barabarani, zikienda maili mia moja kwa saa; kila moja ya hizo, nguvu farasi mia nne au mia tano. Asingeweza kusimamisha moja ya hizo. Lakini acha ainue mkono huo. A-ha. Anayo mamlaka. Hayo ndiyo hufanya breki kulia. Si nguvu zake. Ni malaka yake.

223 Na sisi tunayo mamlaka, kwa Yesu Kristo. Hiyo ndiyo sababu pepo hupiga mayowe. Unaona? Si kwa sababu tuna nguvu, bali tuna mamlaka. Roho Mtakatifu yupo hapa, mamlaka ya Mungu. “Kazi nizifanyazo mimi, nyinyi pia mtazifanya.” “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Ninamwamini Yeye.

224 Sasa tumeketi katika mahali pa Mbinguni, katika Uwepo wa Kristo, tumeinuliwa juu ya masumbuko ya ulimwengu, katika milki ya imani. Ni kitu gani kingeweza kutokea hapa usiku wa leo? Kungeweza kuweko Pentekoste nyingine. Kungeweza kuwa na kitu kama hicho kikitendeka moja kwa moja hapa, usiku wa leo, kama ilivyokuwa katika Matendo 2. Hiyo ni kweli.

225 Kristo yupo hapa. Laiti tungaliweza kuondolea mbali ugumu wa mioyo yetu! Je! Yeye yupo pamoja nasi? Je! hiyo ni kweli? Je! Kristo yuko miongoni mwetu? Aliahidi kuwa. Ungemjua je Yeye? Si kwa jinsi Yeye alivyoonekana, bali kwa kazi ambazo Yeye alifanya. Hilo ndilo Yeye aliloahidi, na Yeye alisema angefanya hilo.

226 Mungu, tusaidie usiku wa leo, kwamba wakati tukitoka hapa, maombi yangu ni . . . Na mimi nitalisema tu huku macho yangu yakiwa yamefumbuliwa, kwenu enyi watu. Ninaomba ya kwamba mtaona kitu fulani halisi sana, kwamba Mungu atafanya jambo halisi sana, usiku wa leo, hata nyinyi mtasema kama wale waliotoka Emau, mnapoenda nyumbani mwenu, “Je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu?” Unaona, walikuwa . . .

227 Yesu alikuwa amesulubiwa, akafa, akazikwa, uvumi ulikuwa umekuwa Yeye alikuwa amefufuka, ndipo Yeye akatembea

pamoja nao siku nzima na wao hawakumjua Yeye. Ametembea pamoja na watu wengi, hawakujua. Huyu ndiye Yule aliyemzuia *yeye* asipatwe na ajali akija hapa; hicho ndicho ambacho humponya mtoto *wako*; Kristo, na labda hukutambua hilo.

²²⁸ Lakini usiku mmoja Yeye aliwafikisha Emau, Kleopa na rafiki yake, nao wakafunga milango, ndipo Yeye akafanya jambo vile tu Yeye alivyolifanya kabla ya kusulubiwa Kwake. Wanajua ilikuwa ni Yeye, katika ufufuo Wake. Upesi walienda kuambia wengine.

²²⁹ Naomba Yeye afanye jambo usiku wa leo, kama Yeye alivyofanya kabla ya kusulubiwa Kwake, kwetu sisi; kusudi sisi, tunapotoka Emau, kwamba tuweze kuwaambia wengine, “Mioyo yetu iliwaka ndani yetu.” Naomba tuweze kuona kitu halisi, si sana fundisho jipya au kitu kingine; bali fundisho, ambalo tunalijua, likiwekwa dhahiri na nguvu za Mungu.

²³⁰ Jana usiku niliitisha mstari wa maombi, wakaja, mama aliyelemaa na kadhalika, wakaponywa. Shuhuda! Kidogo tu; inatubidi tu kuwa hapa kidogo, si vya kutosha hata kukujua. Huko ndani ningeweza kushika hisia za watu, wakisema, “Anasoma mawazo yao.” Nilijaribu kugeuza mgongo wangu kwa watu na kuwaonyesha hakukuwa ni kusoma mawazo.

²³¹ Wengi wenu watu wa zamani hapa Arkansas mnakumbuka wakati nilipokuwa nikishika mkono wa mtu, jinsi Yeye alivyoniambia, “Itakuja kutimia basi, kwamba ikiwa utakuwa mwaminifu, utajua siri hasa ya moyo wao.” Mnakumbuka hilo, nyinyi nyote? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Na mambo ambayo Yeye amefanya, kote ulimwenguni, kila mahali!

²³² Msisahau jarida la *Life* sasa, mwezi uliopita. Kuona mahali ambapo Yeye alibashiri kile ambacho kingetukia, na hapo wakisimama hapo, mashahidi hapa usiku wa leo ambao walikuwa humo ndani. Hata sayansi haijui chochote kuhusu hilo. Wanashangaa ni kwa nini ingeweza kuwa; bali ndivyo ilivyo.

²³³ Sasa, angalia, ninaenda kuchukua Andiko jipya usiku wa leo. Biblia ilisema, kwamba, “Yesu Kristo ndiye Kuhani Mkuu awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.” Je! hiyo ni kweli, ndugu? [Wahudumu wanasema, “Hiyo ni kweli. Amina.”—Mh.] Hilo ndilo Andiko. Sasa, kama Yeye ni Kuhani Mkuu awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, sasa kama ulimgusa Yeye, Yeye angefanya kazi, kama Yeye ni yule yule kama Yeye alivyokuwa, Yeye angetenda kama Yeye alivyofanya wakati ule. Maana huwezi. . . Hiyo ndiyo njia pekee utakayoweza kumjua Yeye, ni kwa kazi Yake. Unaona?

²³⁴ Mnafiki yeyote anaweza kuweka makovu mkononi mwake, na damu au chochote kingine, lakini maisha ndiyo ambayo huonyesha. Unaona? Ningeweza kuchukua mti na kufunganisha

majani kwake, hapa nje, ya mti mwingine, lakini je! hutoa tunda la aina gani? Unaona?

²³⁵ Sasa, Uhai wa Kristo unaishi ndani yako, basi kama Uhai ule wa kwanza uliotoka kwenye hilo tawi. . . Sasa Yeye hana mikono sasa ila yako na yangu. Yeye hana sauti ila yangu na yako. Unaona, mzabibu hauzai tunda. Tawi huzaa tunda. Na kama tawi lililozaa katika tagaa la kwanza lililotokana na shina la mzabibu, kama nilivyosema, waliandika Kitabu cha Matendo nyuma yake. Kama huo ukiwahi kuweka shina jingine la asili, utaandika Kitabu kingine cha Matendo nyuma yake. Itakuwa ni Roho yule yule, maana ni Uhai ule ule katika mzabibu wote. Kila tawi linalozaa litakuwa Hapo.

²³⁶ Sasa ninataka mtambue jambo fulani, tunapoketi hapa. Ni wangapi wenu wanaamini kwamba Kristo yupo hapa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ni wangapi wenu walio wagonjwa, inua mkono wako. Ni wangapi wenu wanaamini kwamba una imani tosha, kwamba ungegusa vazi Lake, Yeye angetenda vile vile?

²³⁷ Siendi kuitisha mstari wowote wa maombi. Kuuita tu, acha tu uje kuanzia hapa. Hiyo ni changamoto kwelikweli. Lakini mna imani nyingi, na mimi ninaamini kwamba Mungu ataiheshimu.

²³⁸ Sasa ninaenda kutazama kwenye kusanyiko, na ninataka kuona kama kuna mtu ninayemjua katika kusanyiko. Ninamjua Ndugu Tracy Boutliere anayeketi hapo. Ndugu huyu hapa, siwafahamu hawa wahudumu moja kwa moja hapa. Mhudumu mmoja huko nyuma kabisa pale ambaye ninamjua. Nje ya hao, juu ya mamlaka ya Biblia yangu, na Hiyo ikiwa juu ya moyo wangu. . . Siapi, maana Biblia ilisema tusifanye hivyo; lakini kwa Biblia yangu ikiwa juu ya moyo wangu, sisemi uwongo. Simwoni mtu mmoja zaidi ambaye ninamjua, nje ya Jim Maguire.

²³⁹ Na kama sina hakika, huyo ni ndugu ambaye nilikutana naye maskanini hivi majuzi. Nilikutana tu na yeye. Ninasahau jina lake. Yeye ni. . . hufanya kazi maskanini huko Jeffersonville. Hiyo ni kweli? Sasa, huyo ndiye mtu pekee nimjuaye, ambaye ninaweza kumwona ambaye ninamjua.

²⁴⁰ Sasa, kama Yesu alikuwa hapa, na wewe ulitaka kuponywa, na ungemwuliza, "Bwana, Wewe utaniponya?"

²⁴¹ Hili hapa ndilo. Kama Yeye alikuwa amesimama hapa amevaa suti hii ambayo Yeye alinipa, Yeye asingeweza kukuponya. Amefanya hivyo tayari. Unaona, ulimalizika pale Kalvari. Na ulimwengu mzima uliokolewa, ulimwengu wote ulisamehewa, kila kitu kilitendeka Kalvari. Unaona, "Yeye alijeruhiwa kwa ajili ya makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tulipona," wakati uliopita. Unaona?

²⁴² Sasa jambo pekee likupasalo kufanya. Halitakufaidi chochote isipokuwa uliamini; si kulihisi. Yesu kamwe hakusema, “Je! ulihisi hilo?” Yeye alisema, “Je! uliamini hilo?”

²⁴³ Nimeona watu wakiinua mkono wao, wanasema, “Hisi hilo! Hisi hilo!” Yeye kamwe hakusema hilo.

Alisema, “Je! uliamini hilo?” Imani, unaona.

²⁴⁴ Angalia, sasa. Kama Yeye ni Kuhani Mkuu yule yule, ingembidi Yeye kutenda kwa njia ile ile. Haijalishi ni kiasi gani Yeye angenipaka mafuta, Yeye hana budi kukutia upako, pia.

²⁴⁵ Sema, ninaona mwanaume ninayemjua. Yule pale Bw. Way, yule mtu aliyeanguka akafa kanisani hivi majuzi, ambaye Mungu alimfufua, ameketi moja kwa moja pale. Na mhudumu ameketi karibu na yeye, ninayemjua, ameketi moja kwa moja pale karibu na yeye. Lakini vinginevyo, hili. . . Naam, ninaamini ninamwona ndugu huyu, huyu ni kaka yake ambaye nilikutana na yeye huko chini pamoja na familia ya Blackwell leo hii, wakiomba nyumbani.

²⁴⁶ Lakini nyinyi watu mnaomwamini Yeye, na mnaamini kwamba mnaweza kumgusa Yeye, ninaenda kuwaulizeni jambo fulani. Sasa, mimi ni ndugu yenu, mwa—mwa—mwanaume tu, kama tu mume wako, au kaka yako, au mchungaji wako, mwanaume tu. Na sasa, hapo, si nje katika chumba fulani chenye giza, kama ibilisi fulani. Pia, ibilisi hafanyi hivyo, kwa vyovyote vile. Hivi uliwahi kusikia ibilisi akihubiri Injili, na kufanya nafsi ziokoke na kuponywa? “Kama Shetani anaweza kufukuza Shetani, basi ufalme wake umegawanyika dhidi yake mwenyewe,” Yesu alisema. La.

²⁴⁷ Lakini papa hapa, wewe tazama na uamini kwamba Yesu angali anabaki Kuhani Mkuu yule yule ambaye Yeye alikuwa, na unasema, “Bwana Yesu, mimi ni mgonjwa. Ama, ninaye mama mgonjwa aliyeketi hapa, ama kaka nyumbani. Bwana, si—si—siwezi kulipa deni yangu. Nisaidie. Nita—nitakiri dhambi zangu zote. Mimi—mimi—mimi ni mwenye dhambi; ni—ninataka kujiweka sahihi na Mungu.” Kitu kingine, mwombe Yeye. Mguse Yeye, kama Kuhani Mkuu, na uone kama Yeye hafanyi leo hii kama Yeye alivyofanya wakati ule. Hiyo inaonyesha kwamba Yeye yuko pamoja nasi.

²⁴⁸ Sasa, ninaamini Yeye atafanya hilo. Sininii...Yeye kamwe hajawahi kunipungukia, katika miaka hii yote. Ni—ninamwamini Yeye. Lakini unaweza kuelewa ni changamoto gani hiyo iliyokuwa. Bali si ninii. . .

Mtu fulani alisema, “Hivi huogopi?” La, bwana.

²⁴⁹ Ninawezaje kuogopa, na Yeye moja kwa moja hapa karibu nami? Yeye, ni Neno Lake; si langu. Mimi ninasema tu kile Yeye alichosema, hayo ndiyo maungamo yangu. *Ungama* maana yake “sema jambo lile lile.” Maandiko, ambayo ni Mungu, Mungu

katika umbo la herufi. “Neno lilifanyika mwili likakaa miongoni mwetu.” Na Neno lingali ni Mungu. Nalo Neno lilisema, “Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.” Ni juu Yake kuthibitisha Hilo. Inastahili mimi niamini Hilo. Sasa wewe amini Hilo.

²⁵⁰ Sasa ninataka kila mmoja wenu basi, kimya, kwa utulivu, kumwomba Mungu, na kusema, “Bwana Mungu, nisaidie. Ninajua maskini yule mwanaume mwenye mabega yaliyoinama anayesimama pale hajui chochote kunihusu mimi, bali Wewe unanijua. Na kama Wewe utafanya tu, na kurudia Maandiko kwa ajili yangu usiku wa leo.”

²⁵¹ Kama yule mwanamke alivyogusa vazi Lake. Yeye kwa kweli hakuhisi mguso wa mkono, kwa sababu, kama nilivyowaambia, vazi la Kipalestina hupwaya; vazi la ndani, zito. Majoho makubwa mazito, Yeye hakuhisi huo. Ndipo Yeye akasema, “Ni nani aliyenigusa Mimi?”

²⁵² Naye Petro akamkemea, akisema, “Bwana!” Mbona, alimchukua Yeye na kumkemea kwa ajili ya hilo. Kwa maneno mengine, “Linasikika la kiwazimu Kwako kusema hilo. Kila mtu ameweka mikono yao kukuzunguka Wewe, wakikupapasa Wewe mgongoni. ‘Nani aliyenigusa Mimi?’”

²⁵³ Yeye akasema, “Lakini nguvu zimenitoka Mimi. Mtu fulani amenigusa Mimi kwa mguso tofauti.”

Je! unaweza kufanya mguso huo usiku wa leo?

²⁵⁴ Ninajisalimisha mwenyewe. Sasa kumbukeni, mimi ni bubu kabisa kwa mambo haya, nje ya Ufalme wa Mungu. Ni kama tu vile kipaza sauti hiki. Kipaza sauti hiki hakiwezi kunena; kinaweza tu kunena wakati kitu fulani kinanena kupitia kwake. Na sisi ni kama tu hicho kipaza sauti, kwa hili. Sikujui wewe, bali inachukua kitu fulani kuongea kupitia hapa.

²⁵⁵ Na wewe amini hilo, na uwe na imani kwa Mungu, na Mungu atajalia hilo. Je! mnaamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa aminini tu. Iweni na imani, na msitie shaka. Mwaminini Bwana Mungu. Sasa ombeni tu, mwe na kicho kabisa, na mwone tu.

²⁵⁶ Sasa, Baba wa Mbinguni, nimekuwa nikizungumza kirefu. Wapo watu walioketi hapa ambao ni watu wanaoelekea Umilele, kila mmoja wetu. Vichwa vyetu vimeinamishwa kuelekea mavumbini, ambapo Wewe ulituchukua kutoka; na ikiwa Wewe utakawia, tutarudi kwenye hayo mavumbi. Roho hizi na nafsi zilizoko ndani yetu, hazina budi kurudi Kwako kwa ajili ya Hukumu.

²⁵⁷ Sasa, Baba wa Mbinguni, tunaomba ya kwamba Wewe utaliheshimu Neno Lako usiku wa leo. Nimezungumza kukuhusu Wewe, sasa nena kwamba nimesema Kweli, Bwana. Mimi ni mtumishi Wako. Ninajikabidhi Kwako. Na iwapo kuna mtu hapa ndani, Bwana, aliye na aina hiyo ya imani, inayoweza

kuleta madhihirisho ya Yesu Kristo; kuonyesha ya kwamba ishara ambayo Yeye aliahidi, ishara ya mwisho kwa kanisa la Mataifa, itafanyika; kanisa teule, kama kundi la Ibrahimu, walioitwa watoke. Tunamwona Billy Graham na wale watu chini huko Sodoma, wakiwaita watoke; lakini tunamkumbuka Yule ambaye alikaa na Ibrahimu akawapa ishara nyingine, kwamba mwana aliyekuwa anakuja alikuwa amekaribia. Bwana, jalia tuione ishara hiyo, usiku wa leo, kama vile Mtu huyo alivyokuwa amegeuza mgongo Wake kuelekea kwenye hema, na kasema, “Ni kwa nini Sara akacheka?” Yesu alisema itajirudia tena, kabla tu ya kuja kwa Mwana wa Adamu; Mungu akidhihirishwa katika mwili, katika mwili wa binadamu, kupitia uweza wa Roho Mtakatifu na Damu ya Yesu Kristo. Tujalie, Bwana. Ninakabidhi hii, mimi mwenyewe, Kwako kwa ajili ya utumishi Wako. Nena, Bwana. Watumishi wako wanasikiliza.

²⁵⁸ Sasa, katika Jina la Yesu Kristo wa Nazareti, ninachukua kila roho hapa ndani chini ya udhibiti wangu, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, kwa ajili ya kazi Zake.

²⁵⁹ [Mtu fulani anaanza kuongea katika lugha nyingine. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . ? . . .

²⁶⁰ Sasa acha Roho Mtakatifu afanye kazi. Sasa je! mambo niliyosema ni sahihi, au si sahihi? Je! Yeye angali anabaki Kristo? Je! alitimiza ahadi Yake, ya, “Popote watakapokutanika wawili au watatu, nitakuwa hapo katikati yao”? [Kusanyiko linasema, “Amina.”] “Kitambo kidogo, na ulimwengu huko nje hautaniona Mimi tena, hata hivyo nyinyi mtaniona Mimi, kwa kuwa Mimi” (kiwakilishi cha binafsi) “nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu. Kazi nizifanyazo mimi, mtazifanya pia; nyingi kuliko hizi, kwa kuwa ninaenda kwa Baba.” Je! ni kweli? [“Amina.”]

²⁶¹ Ninaiona hiyo Nuru ikining’inia juu ya maskini, msichana mweusi pale. Yeye anapata nafuu. Kumbukeni tu, anaenda kuwa mzima. Unatoka mahali mbali na hapa. Inakubidi kujinyima ili kufika hapa kila usiku, lakini usiwe na hofu kuhusu mtoto huyo. Umepata neema kwa Mungu. Huyo aliitwa, hivi majuzi usiku. Amini tu.

²⁶² Hapa, je! mtu yeyote ameiona hiyo Nuru? Inua mkono wako kama umeiona. Umeona picha Yake. Hivi hamwioni Hiyo? Tazameni hapa. Tazameni hapa. Nuru hiyo, yenye rangi ya kaharabu, imesimama papa hapa. Hivi hamwioni Hiyo? Inasonga, papa hapa.

²⁶³ Iko juu ya mwanamke. Mwanamke huyo anaugua kisukari. Ameshaomba. Anaamini. Mungu, usiache Hiyo imwondokee. Anaenda kuikosa Hiyo, kwa hakika. . . Bibi Davis, amini kwa moyo wako wote. Haya basi.

²⁶⁴ Sijawahi kumwona mwanamke huyo, maishani mwangu. Hii hapa mikono yangu mbele za Mungu. Mwulize kama mambo hayo. . . Je! hiyo ni kweli, mama? Punga mikono yako, namna

hii, kama hiyo ni kweli. Sasa alingusa Nani? Si mimi, yuko yadi ishirini kutoka kwangu. Bali alingusa Kuhani Mkuu, Yesu Kristo. Kuwa tu na imani. Usitie shaka. Je! unaamini?

²⁶⁵ Hapa, angalia hapa tena, papa hapa. Mwanamke fulani anaomba. Anaugua ugonjwa wa tumbo, shida fulani na miguu yake. Ee Mungu! Bibi Cotton, amini kwa moyo wako wote. Pokea uponyaji wako, Yesu Kristo anakufanya mzima.

²⁶⁶ Mungu Mbinguni anajua sijawahi kumwona mwanamke huyo maishani mwangu. Mwanamke huyo aligusa nini? Huyu si ni yule yule Kuhani Mkuu? Ni kwa nini una shaka? Usitie shaka. Mwamini Mungu.

²⁶⁷ Mtu fulani nyuma katika wilaya hii. Wewe omba. Amini. Yeye ni Mungu, kila mahali.

²⁶⁸ Kuna mama aliyeketi hapa akiomba. Hajiombezi mwenyewe. Anaomba kwa ajili ya mwanawe. Huyu ana tatizo la tumbo. Hayuko hapa. Yuko katika jimbo jingine. Anatoka katika mji uitwao Pontiac, Michigan. [Dada huyo analia, “Loo!”—Mh.] Usiogope. Alikuwa na tumbo lenye vidonda, kutokana na hali ya wasiwasi. Vimemwacha. Amina. Imani yako ilingusa Yeye.

²⁶⁹ Kusudi mweze kujua. Hapa ameketi mwanaume hapa, yule ambaye huipiga hii gitaa, chochote kilicho hapa, anaugua tatizo la tumbo, pia. Ibilisi alifikiri alipita na hiyo, lakini hakupita. Umeponywa, bwana. Yesu Kristo anakufanya mzima.

²⁷⁰ Je! unaamini kwa moyo wako wote? “Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana.”

Je! unaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

²⁷¹ Jamaa mdogo aliyeketi hapa, akiomba kwa ajili ya mke wake, huku ameinua mikono yake. Mke anaugua ugonjwa wa pumu. Kama unaamini kwamba Mungu atamponya, ndugu, huyo mke atapona. Amina.

²⁷² “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Waulizeni watu hao, sijawahi kuwaona maishani mwangu.

²⁷³ Nyuma kabisa hapa ameketi mwanamke mwingine. Yeye ana kivimbe kwenye titi. Loo, naomba asiukose! Bibi Patterson, kubali uponyaji wako. Simama kwa miguu yako, mpe Mungu utakufu. Vema. Sijawahi kumwona mwanamke huyo, maishani mwangu; Mungu Mbinguni anajua hilo.

²⁷⁴ Vipi kuhusu hao walio kwenye machela hapo chini? Vipi kuhusu yule mwanamke pale? Inamisha kichwa chako, mwanamke. Hapo ameketi mwanamke ameketi pale, yuko kwenye kitanda cha wagonjwa. Je! unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, mtumishi Wake? Ipo Nuru inayoning’inia juu ya mama huyo. Anaugua ugonjwa wa moyo. Kama ukikaa hapo, utakufa. Simama, katika Jina la Yesu Kristo. Chukua kitanda chako na uende nyumbani, na wewe utapona ugonjwa wako wa moyo.

275 Je! unamwamini Mungu? Ni wangapi wenu wanamwamini Yeye? [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Sikiza, rafiki yangu. Aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa, Kuhani Mkuu awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Je! unamwamini Yeye? [“Amina.”] Kama hiyo si kazi ambayo Yesu Kristo alijithibitisha kwayo kuwa Masihi! Je! hayo ndiyo Maandiko yasemayo? Semeni, “Amina.” [“Amina.”]

276 Pia jambo lingine, wewe, wewe unakabiliwa na kurukwa akili. Ondokea hilo. Kimbilia maisha yako. Kimbia upesi. Yaache mambo yaliyopita katika wakati uliopita, na umtazame Mungu. Wewe ni mhudumu wa Injili. Wewe, nilizungumza na wewe asubuhi ya leo. Hukujua kilikuwa ni kitu gani, nami sikujuu kilikuwa ni kitu gani, bali ninakiona sasa. Unakaribia kurukwa akili. Ibilisi anaweka kila kitu niani mwako, akijaribu kukufanya kugeuka dhidi, hata dhidi yangu. Hiyo ni kweli. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Sahau hilo. Mwambie yeye ni mwongo. Ukubali sasa hivi, na huo utakuacha na hautarudi tena. Utakuwa mtu huru.

277 Ninakusai kuamini mambo haya! Mtu huyo alinijia asubuhi ya leo, akiuliza. Sikujua, bali ninakiona. Papa hapa kipo mbele zake, angalia kivuli hicho cheusi kinachoingia tu na kutoka. Lakini sasa kitu hicho kimemwacha. Hiyo ni kweli. Haleluya. “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.”

278 Wakati Roho Mtakatifu akiwa hapa, hizi hapa lesa. Hebu tuombe, huku mkishikilia katika maombi.

279 Baba wa Mbinguni, tumefundishwa katika Biblia, kwamba walichukua kutoka kwa mwili wa Mtakatifu Paulo, lesa na nguo, roho chafu ziliwatoka watu, na wao waliponywa. Na huku tukiutambua uwepo Wako hapa, tunatambua kwamba sisi si Mtakatifu Paulo, lakini Wewe ungali Yesu. Na haikuwa ni yeye, katika mwanzo, ilikuwa ni Wewe; imani ndani ya watu, wakati walipomwona akitabiri na kujua kwamba Mungu alikuwa pamoja na Yeye. Bwana, Wewe yaheshimu maombi ya watu hawa tena leo hii, kwa njia ile ile.

280 Mwandishi mmoja alisema, “Wakati Israeli walipokuwa njiani mwao kuenda nchi ya ahadi, kwamba Bahari ya Shamu iliwakatilia, moja kwa moja katika njia ya wajibu, kuenda kwenye nchi ya ahadi. Ndipo Mungu akaangalia chini kupitia ile Nguzo ya Moto, kwa macho yenye hasira; Bahari ya Shamu ikaogopa, ikarudi nyuma, na Israeli wakaendelea hadi nchi ya ahadi.”

281 Mungu, usiku wa leo, watu wanaitaka ile ahadi, “Juu ya mambo yote ninataka mnawiri katika afya njema.” Na ugonjwa umewakatilia mbali. Naomba Wewe utazame chini usiku wa leo kupitia Damu ya Yesu Kristo, na wakati lesa hizi zinapowekwa juu ya wagonjwa, katika ukumbusho wa upako huu mkuu wa Roho Mtakatifu, wa Kristo akijidhihirisha Mwenyewe hapa

kupita kivuli chochote cha shaka, Yesu yeye yule akituonyesha kwamba Yeye angali hai na alifufuka kutoka kwa wafu. Jalia ugonjwa utishwe wakati ishara hizi zinapowekwa juu ya wagonjwa, hebu akimbie kurudi nyuma na kuondoka, na watu waponywe, kupitia Jina la Yesu Kristo.

²⁸² Kwa utulivu. Biblia ni sahihi. Na kama Yesu yuko radhi kuja hapa na kudhihirisha hili sana kwenu, kikamilifu sana, kupita kiwango chochote cha saikolojia, kupita kiwango chochote cha mhemko, muujiza mkamilifu! Muujiza ni kitu ambacho hakielezeki. Ninaweza kuona ambapo mtu angeweza kuwa ki—kidogo amelemaa kwenye mguu wake, na angeweza kuruka, na chini ya mhemko. Kweli. Lakini ni nani angeweza kumwambia kile ambacho amefanya, na mahali ambapo ametoka, na kile ambacho kimefanyika, na kile ambacho kitakuwa? Na mimi ninawapa changamoto; haijakosa wakati wowote, katika makumi ya maelfu mara maelfu, kote ulimwenguni. Hakuna . . .

²⁸³ Tuna uigaji mwingi, ninajua hilo. Huo hauna budi kuja, uigaji wa kimwili. Lakini huo haunini . . . Huo hufanya tu Kitu halisi kung’aa vizuri zaidi; huo humfanya Yesu Kristo kuwa halisi.

²⁸⁴ Yeye huyu hapa usiku wa leo! Yuko miongoni mwetu, Roho Mtakatifu yeye yule ambaye mlimpokea, na Yeye huwaacha mnene kwa lugha na kufanya mambo ambayo mmefanya. Roho Mtakatifu yuyo huyo akiwapa ishara hiyo ya Sodoma, kuondoka kwenye upuuzi kama huo, wakati wa kuteketezwa kwa ulimwengu huu umekaribia. Bomu limewekwa huko likiwa na namba juu yake. Mkimbilieni Kristo, upesi.

²⁸⁵ Yeye pia alisema, katika Maandiko, maneno ya mwisho yaliyoanguka kutoka midomoni Mwake, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya.” Je! mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

²⁸⁶ Ninaenda kuona kama mnaamini hilo? Ninashangaa ikiwa tungeweza kupiga mbio vizuri, mtindo wa kale, mstari wa mbio wa Arkansas hapa, kwa dakika moja. Hivi mnaweza kuamini hilo? Je! mngependa kuona hilo, mikono ikiwekwa juu yenu? Je! mngependa kuwa na hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

²⁸⁷ Sijui jinsi tutakavyoliendesha. Nina shaka kama tungeweza kufanya hilo. Hivi mnalitilia shaka? Je! mnafikiri tungeweza? [Ndugu Samuel Johnson anasema, “Ninaamini tunaweza. Amina.”—Mh.] Sijui jinsi tutakavyofanya. Lakini tunaweza kujaribu, kama mtakuwa na kicho.

²⁸⁸ Hebu wale walio humo ndani . . . Kitu gani? Sehemu kwa sehemu. Vema, hebu wale walio kule nyuma, walio na hizo kadi za maombi, wajitokeze moja kwa moja mbele katika mstari huo hapo. Sehemu ya kulia.

²⁸⁹ Sasa ninawatakeni mjue, ndugu zangu, dada, kwamba haiwabidi kungojea mwinjilisti fulani maalum kuja huku. La,

la. Mchungaji wenu ana kitu kile kile. Sasa, yeye—yeye—yeye hueda asiweze ku—kuwa na karama hiyo ya unabii; hiyo huja moja kwa kizazi. Lakini, tazama, anazo haki hizo hizo kukuombea ambazo ningekuwa nazo. Upambanuzi huo haukuponyi; hukufanya tu umtambue Mungu, kwamba uko katika Uwepo wa Mungu.

²⁹⁰ Bali mwinjilisti anaenda mjini, anafanya maombi yote, kubatiza kwote; ndipo watu, wakati akiondoka, mchungaji ni . . . Vema, watu wanafikiri mchungaji wao si kitu. Mchungaji wenu ni mtu wa Mungu. Amewaongoza salama umbali huu; anaweza kuendelea nanyi. Yeye ni mtu wa Mungu aliyeagizwa.

²⁹¹ Na mimi ninawatakeni, kila mmoja wenu, ukija kupitia mstari huu wa maombi na huamini hili, kaa mbali nao; utakuwa mbaya zaidi. Lakini ikiwa kwa kweli utaamini, unapopita chini ya mikono iliyotiwa upako ya Mungu, ninawatakeni mwende nyumbani mkishuhudia kwa nguvu za Mungu; utoke hapa, ukipaza sauti na kumsifu Mungu, kwamba yote yamekwisha. Ninawatakeni mfanye hivyo.

²⁹² Ninawataka hawa wachungaji wanisaidie. Loo, Ndugu Moore, na Ndugu Hooper, na wengi wa ndugu hawa hapa ninaowajua, na kundi hili zuri la wachungaji hapa, simameni tu na mnifanyie tu mstari mdogo moja kwa moja hapa. Hivi ndivyo tulivyolifanya. Sijafanya hili kwa miaka. Lakini wakati Roho Mtakatifu angali juu yangu, (ndio kwanza nione jambo fulani likitendeka basi), wakati Yeye angali hapa, na wakati nikiweza, na wakati . . . Wanao upako ule ule na mamlaka yale yale. Ni hayo tu. Tunaenda kuweka mikono juu ya wagonjwa. Nayo Biblia ilisema, “Wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya.” Biblia ilisema hivyo. Hilo ni Neno la Mungu. Njoni hapa nje, ndugu, njoni hapa nje na mfanye mstari moja kwa moja hapa. Ninaenda kusimama na ndugu hawa.

²⁹³ Sasa, mkitoka, enyi watu mahali hapa, mnapoenda nje, toka moja kwa moja nje ya jengo, rudi moja kwa moja ndani tena. Na sasa ninaenda kuuliza mtu fulani asimame hapa, labda maskini ndugu yule hapa, maskini . . . Njoo hapa, na wewe uangalie mistari hii, ukiweza, au ndugu fulani anayeweza kusimama hapa na kuwaita kwa sehemu.

²⁹⁴ Hebu wahudumu sasa, wahudumu, watumishi wa Yesu Kristo waliopakwa mafuta, wasimame tu moja kwa moja hapa.

[Mtu fulani anasema, “Ndugu Jackson na Ndugu Ruddell.”]

²⁹⁵ Nina ndugu kadhaa hapa ambao wanatoka Jeffersonville, baadhi ya rafiki zangu kutoka maskini makanisa tunaoshirikiana nao kutoka Maskanini. Ndugu Don Ruddell, mafanikio makubwa katika kuwaombea wagonjwa. Don, upo hapa? Ndugu Junior Jackson, mhubiri wa Kimethodisti ambaye ndio kwanza nimbatize katika Jina la Yesu Kristo. Alipokea Roho Mtakatifu. Huyu mwingine alikuwa mhudumu wa church

of God. Ninawatakeni enyi ndugu ambao huwaombea wagonjwa, karibu na Maskani, njoni, msimame katika mstari huu pamoja na ndugu hawa.

²⁹⁶ Hiyo ni sawa, sivyo, ndugu? Hiyo ni sawa, sivyo? Hakika. [Ndugu hao wanasema, “Hakika!”] Naam. Vema, njoni, simameni karibu.

²⁹⁷ Yu wapi Ndugu Willard Collins? Mhudumu mwingine, mhudumu wa Kimethodisti, ndio kwanza apokee Roho Mtakatifu, na kubatizwa. Ningependa aje.

²⁹⁸ Maskini mvulana wake, hivi majuzi, alikuwa akifa kwa—kwa homa ya baridi yabisi, naye daktari akasema hata usimwache ainue kichwa chake vya kutosha kuweka mpira kinywani mwake. Nilikuja kutoka Tucson, kuhubiri *Mihuri Saba*. Na wakati alipofanya hivyo, alimchukua mtoto huyo kutoka kitandani na kumleta huko. Na punde tu alipoingia, Roho Mtakatifu akasema, “BWANA ASEMA HIVI. Mpeleke mtoto huyo nyumbani, amepona. Atacheza na mvulana wangu mdogo.” Huyu hapa ndugu huyo amesimama moja kwa moja hapa sasa. Mke wake yuko hapa ndani.

²⁹⁹ Nadhani Mike ameketi hapa, mwenyewe. Kweli. Uko wapi, Mikey, uko wapi? Ndipo madaktari . . . Yule pale; fumbo. Daktari alisema leta . . . Wakuu wa afya walimpeleka mtoto huyo ndani mbio. Daktari akaenda na kumchunguza; akakuna kichwa chake, kasema, “Hakuna hata chembe moja ya huo ndani yake.”

³⁰⁰ Ni kitu gani? Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele!

³⁰¹ Marafiki, sababu niliwaita wanaume hawa. Wao ni wahudumu. Wao ni wachungaji. Wao ni watu walioitwa kuwaombea wagonjwa, sawa na mimi au mtu yeyote mwingine. Na mimi ninawatakeni mjue kwamba mchungaji wako ana mamlaka kufanya hili. Haikubidi kumngonjea Oral Roberts, au Jack Jones, au mimi, ama mtu yeyote mwingine. Yesu Kristo yuko kila mahali; wewe mwamini Yeye. Mchungaji wako ameitwa kufanya hilo. Ikiwa hujawahi kubatizwa; baada ya mkutano huu, shauriana na mchungaji wako, ujiweke vizuri na Mungu. Kama hujapokea Roho Mtakatifu, nenda kanisani mwake, atakuelekeza juu ya jambo la kufanya.

³⁰² Sasa wakati unapopita, omba. Na mimi ninataka kila mtu hapa ndani, kila mtu binafsi, ninataka uombe. Ninataka utembe tu taratibu kupitia mstarini. Ninaenda kusimama moja kwa moja hapa pamoja na kundi hili la wanaume, tukiweka mikono juu ya watu hawa. Mchungaji huyu anaenda kusimama hapa na kuita safu. Na wakati ukipita, na mikono hii iliyotiwa upako . . . Ninaenda kukuombea sasa, na wao wanaenda kukuombea.

³⁰³ Basi wakati wakiweka mikono yao juu yako, kumbuka, ni kwamba, umeponywa tu kama vile ungeokolewa. Biblia, Hiyo ilisema, “Tubuni, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo

kwa ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.” Hiyo ni ahadi ya Mungu. Yeye atafanya hivyo kama ukiamini. Lakini usipoamini, haitafanya kazi. Na Yeye alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Imefanyika, wakiweka mikono yao juu yako, kama unaamini hiyo.

³⁰⁴ Je! mnaamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Je! mnaamini, usiku wa leo, kwamba mmeona mengi halisi kama tu yule mama kulungu alivyoweza kutoa, kumwona Yesu Kristo akijidhihirisha Mwenyewe miongoni mwetu? Kama mnaamini Yeye yupo hapa, semeni, “Amina.” [“Amina.”] Basi, Huyu hapa.

³⁰⁵ Hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa. Sasa hili hapa ombi langu kwa ajili yenu, kwa moyo wangu wote.

³⁰⁶ Baba wa Mbinguni, ninakupenda Wewe. Wewe ni Uzima wangu. Wewe ni matumaini yangu, Mungu wangu, Mfalme wangu, Mponyaji wangu, Mhifadhi wangu. Si hayo tu, bali ninadhihirisha hisia za kila Mkristo mwaminio hapa ndani, hilo ndilo ulilo Wewe.

³⁰⁷ Hapa anasimama mwanamume, baadhi yao wanasimama hapa wenyewe, wagonjwa. Ninajua ni wagonjwa. Nilionga Roho Wako akining’inia juu yao, dakika chache zilizopita. Nikiwajua hao wahudumu wagonjwa, bali mioyo yao inaendea kusanyiko lao, watu; wakiacha mahali pao wenyewe, kusimama hapa katika mstari wa maombi, kuombea kondoo wao. Mungu, mbariki mtu huyo, mbariki kila mmoja wao.

³⁰⁸ Tunaposimama hapa kama mwakilishi Wako, usiku wa leo, wa Kweli hii, Kweli ya Biblia, jalia kila mmoja wa watu hawa awe na upako sana, na Roho Mtakatifu atanini... Wakiweka mikono yao juu ya watu, kwamba kuwe na imani hivi kwamba itamgusa mtu huyo mpaka wao watakubali kipawa kilichotolewa na Mungu cha uponyaji ambacho Wewe umewaahidi, Bwana. Pia jalia kila mmoja anayepita, achochewe sana na matumaini, hata watajua kwamba wanapita chini ya kivuli cha msalaba, ambapo Damu ya Yesu Kristo hupatanisha kwa ajili ya maungamo yao, na Uwepo Wake mkuu hapa pamoja nasi sasa, ambao unathibitisha kwamba Yeye hajafa, Yeye amefufuka kutoka kwa wafu, na anaishi miongoni mwetu. Basi mioyo yetu itawaka tunapoenda kwenye makao yetu mbalimbali, usiku wa leo, tukisema, “Je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo Yeye aliponena nasi njiani?” Ninaomba kwamba Nguvu Zako zitaleta imani hivi kwamba katika dakika hizi chache zijazo, kwa watu hawa wagonjwa, kwamba hakutakuwa na mtu mnyonge miongoni mwetu.

³⁰⁹ Ninampa changamoto kila ibilisi ambaye amewafunga watu hawa, juu ya mamlaka ya Neno la Mungu, na Uwepo wa Yesu Kristo Yule aliyemwaga Damu Yake, kufanya kila Neno halisi kwa kila mtu ambaye ataamini. Shetani, wewe umeshindwa,

wakati wako umewadia, waache watu hawa, katika Jina la Yesu Kristo. Toka miongoni mwao! Tunaendesha kazi ya Mungu, kwa kuweka mikono juu ya wagonjwa, na wao watapona.

³¹⁰ Samuel, imba *Amini Tu*. Anzisha mstari wa maombi. [Ndugu Samuel Johnson anaanza kuimba *Amini Tu*—Mh.] Kila mtu katika maombi sasa. Kila mtu, maombi.

³¹¹ [Ndugu Branham na wahudumu wanaomba na kuweka mikono yao juu ya watu wanapotembea kupitia mstari wa maombi, huku Ndugu Johnson akiendelea kuongoza kusanyiko katika kuimba *Amini Tu* mara nyingi. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ushirika wa nia moja
Ni kama ule huko Juu.

Wakati tunapoachana,
Hutupa maumivu ya ndani;
Bali tungali tutaunganishwa moyoni,
Na kutumaini kukutana tena.

³¹² Baba wa Mbinguni, katika Jina la Bwana Yesu, naomba hili, huu uhusiano na mikono ya kila mmoja, ndugu wahudumu, kwamba Neno la Mungu. Jalia kwamba nguvu zilizomfufua Kristo kutoka kwa wafu, na zimemdumisha Yeye pamoja nasi kwa miaka hii elfu mbili, jalia zifungamanishe. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . nafsi kwa ajili ya Umilele, pia naomba Hizo ziponye ugonjwa miongoni mwetu. Na ninaomba Jina la Yesu Kristo. . . ? . . . Leso hizi na vifurushi hivi, naomba kwamba nguvu za Mungu zitulie juu yake, kupitia Jina la Yesu Kristo. Amina.

³¹³ Sasa hebu kusanyiko lote, mnaoamini kwa moyo wenu wote, kwamba Yesu Kristo ameninii, atatimiza Neno Lake. . . Kama Yeye alitimiza Neno Lake kwa miaka elfu mbili, na kusema hili lingetukia katika wakati wa mwisho, na hapa limefanyika, Yeye atatimiza Neno Lake ambalo lilisema, “Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, hao watapata afya.” Je! mnaamini hilo? Mnalikubali? Basi hebu tuinue mikono yetu pamoja na kumpa Mungu sifa. . . ? . . .



ALIYE MKUU KULIKO SULEMANI YUPO HAPA SWA63-0628E

(A Greater Than Solomon Is Here)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Ijumaa jioni, terehe 28 Juni, 1963, katika Associated Brotherhood Of Christians Campground kule Hot Springs, Arkansas, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2019 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org